JARIDA TOLEO LA OKTOBA - DESEMBA 2022

HALMASHAURI YA WILAYA ARUSHA DISTRICT COUNCIL

# FAHARI YETU

## HALMASHAURI YA ARUSHA

Arusha DC KaziInaendelea........

# ASANTE Dkt. SAMIA SULUHU HASSAN



"Kisongo Maji yatapatikana"

HALIUZWI

# TAHARIRI

## KUBORESHA MIUNDOMBINU KISEKTA NI KUIMARISHA HUDUMA ZA JAMII



Ni ukweli usiopingika uwepo wa miundombinu stahiki kulingana na mahitaji ya wananchi ni kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii kwa wepesi na kwa haraka.

Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, imejikita katika kuboresha miundombinu katika sekta ya elimu, afya, maji na barabara lengo likiwa ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma za jamii kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa huduma muhimu na bora za kijamii katika maeneo yao muda wote.

Halmashauri ya Arusha ni miongoni mwa halmashauri nchini inayonufaika kwa kuletewa fedha kutoka serikali kuu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa miundombinu.

Katika kipindi cha robo ya pili ya Oktoba mpaka Desemba, mwaka wa fedha 2022/2023 tumepokea jumla ya shilingi Bilioni 1.27 kwa ajili ya kutekeleza miradi kisekta.

Katika fedha hizo, halmashauri ilipokea kiasi cha shilingi milioni 507.2 fedha za serikali kupitia Mfuko wa maendeleo ya Jamii (TASAF) ambazo zimeelekezwa kutekeleza miradi 6 ikiwemo ujenzi wa Nyumba ya Mtumishi (2 in 1) Zahanati ya Likamba, ujenzi wa Nyumba ya Mwalimu (2 in 1) Shule ya Msingi Imbibya, ujenzi wa Zahanati kijiji cha Engutoikoit, ujenzi wa Zahanati kijiji cha Lemugur, ujenzi wa Maabara za masomo ya Sayansi shule ya sekondari Oldonyowas, pamoja na ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na matundu 6 ya vyoo shule ya Msingi Olkejulendet.

Aidha halmashauri ilipokea shilingi milioni 760 fedha za nje ya bajeti kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 38 vya madarasa kwa shule 18 za sekondari, madarasa ambayo ni maalum kwa ajili ya mapokezi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza wanaoanza masomo Januari 2023.

Miradi yote hiyo inakwenda kuboresha huduma za jamii pamoja na kusogeza upatikanaji wa huduma hizo karibu na wananchi.

Seleman H. Msumi
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Arusha



# MHE. RAIS SAMIA AWAAHIDI MAJI WANANCHI WA KISONGO

**Na Elinipa Lupembe**

Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amewaahidi wananchi wa Kisongo kuwasiliana na Wizara ya maji kuona namna ya kuunganisha mradi wa maji wa bilioni 600 wa Jiji la Arusha ili kuwafikia wananchi hao.

Mhe. Rais ameyasema hayo kwenyeMkutano wa Hadhara, uliofanyika kwenye soko la Kisongo kata ya Mateves, Halmashauri ya Arusha, wilaya ya Arumeru, wakati akiwaaga wananchi wa mkoa wa Arusha mara baada ya kumaliza ziara yake mkoani humo.

"Tumemaliza tatizo la maji Jiji la Arusha kupitia mradi wa maji wa Bilioni 600, mahitaji ya Jiji la Arusha ni lita milioni 90 tu, na maji hayo yamezidi, tutafanya mpango kuhakikisha maji hayo yanaunganishwa hapa, ili wananchi wa Kisongo mpate maji, Kisongo maji yatapatikana". Amesema Mhe. Rais

Mhe. Rais amewahakikishia wana Kisongo maji na kuongeza kuwa Wizara ya maji inatekeleza miradi mingi kwa sasa, ikitokea bakaa yoyote ipelekwe Arumeru ili kumaliza tatizo hilo.

Katika mkutano huo, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi, Mhe. Noah Lembris alipata fursa ya kuwasilisha changamoto zinazowakabili wananchi wa Jimbo hilo ikiwemo miundombinu ya barabara za ndani, maji, ujenzi wa soko la Kisongo pamoja na mpaka wa mita 200 kati ya Arusha DC na Jiji la Arusha.

Aidha Mhe. Mbunge licha ya kuwasilisha changamoto hizo amemshukuru na kumpongeza Mhe. Rais kwa serikali kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo jimboni humo.

"Kupitia TARURA tumepokea bilioni 1.5 za ujenzi wa barabara za ndani, umesaini mkataba wa bilioni 22 za ujenzi wa barabara ya lami Km 18 Mianzini, Timbolo-Ngaramtoni, bilioni 1,4 za kukamilisha vituo vya afya, milioni 450 kumaliza zahanati 11 lakini pia tumepokea milioni 760 za ujenzi wa madarasa 38 shule 18 za sekondari kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza 2023". Amebainisha Mhe. Noah.

Hata hivyo Katibu Mkuu TAMISEMI Prof. Riziki Shemdoe ameitaja mikakati ya ujenzi wa barabara za ndani katika halmashauri hiyo na kusema kuwa serikali itazingatia mahitaji yaliyowasilishwa na kuweka kwenye mpango wa bajeti kwa mwaka ujao wa fedha.

"Ujenzi wa soko ni mradi mkakati, nitamuelekeza Mkurugenzi wa halmashauri ya Arusha, kuandika andiko likikidhi vigezo, tutakaa na Wizara ya fedha ili mradi huu uanze". Amesema Katibu mKuu huyo.

Hata hivyo Mhe. Rais ametumia fursa hiyo kuwaaga wananchi wa Arusha na kuweka wazi kuwa atarudi Arusha kwa kuwa, Arusha ni kiini cha shughuli za Serikali na Mataifa ya nje.







# RC ARUSHA ASHUHUDIA UTIAJI SAINI MIKATABA 18 YA UJENZI WA BARABARA

**Na Elinipa Lupembe**

Jumla ya mikataba 18 yenye thamani ya shilingi bilioni 4.07 imesainiwa na wakandarasi wa kutengeneza barabara za mkoa wa Arusha, huku Mkuu wa Mkoa huo Mhe. John Mongella akiwataka wakandarasi waliosaini mikataba hiyo, kufanya kazi kwa weledi, uzalendo na kuzikamilisha kwa muda uliopangwa kulingana na mikataba hiyo.

Mhe. Mongella ameyasema hayo wakati akishuhudia utiaji saini wa mikataba kati ya Wakala wa barabara vijijini na Mijini ( TARURA) na wakandarasi 18 watakaofanya matengenezo barabara kwenye halmashauri za Mkoa wa Arusha.

"Tumesaini mikataba, wakandarasi tambueni fedha hizi ni za Umma, ni kodi za wananchi, Serikali imewaamini na kuwapa kazi, nendeni mkatengeneze barabara zenye viwango, vinavyoendana na tahamani ya fedha na kukamilisha ujenzi kwa wakati kulingana na mikataba mliyoisaini" . Amesisitiza Mkuu huyo wa mkoa.

Aidha Mongela amebainisha kuwa kukamilisha barabara hizo kwa wakati na kwa viwango kutasaidia kusogeza huduma kwa wananchi pamoja na kushusha gharama za maisha kwa wananchi na kuharakisha maendeleo binafsi na ya Taifa kwa ujumla na kuwaelekeza TARURA kuhakikisha wanawasimamia wakandarasi hao kwa ukaribu zaidi ili kazi zifanyike kwa wepesi na kukamilisha miradi hiyo kulingana na mikataba yao sambamba na kuendelea kusimamia miradi ya barabara ya zamani ili nayo iweze kukamilika haraka.

Naye Katibu Tawala Mkoa wa Arusha Missaile Musa amesema, kuwa kitendo cha wakandarasi kusaini mikataba hadharani kitasaidia wananchi kuwafahamu wakandarasi watakaoenda kufanya kazi katika maeneo yao.

Meneja wa TARURA Mkoa wa Arusha Lynas Sanya amesema kwa mwaka wa fedha 2022/2023 wamepatiwa jumla ya shilingi bilioni 4.07 kwa ajili ya matengenezo ya barabara kwa awamu ya pili huku awamu ya kwanza ikipokelewa shilingi bilioni 14 na jumla ya shilingi bilioni 18.07 na jumla ya mikataba 34 ilisainiwa.

Naye, Mkandarasi Rashidi Sevingi kutoka kampuni ya Raly (EA) Limited ameahidi kwenda kufanya kazi kwa weledi kwa kuzingatia mikataba waliyosaini na kuwasihi wakandarasi wote kufanya hivyo ili Serikali iendelee kuaminiwa zaidi na kuendelea kuwapa kazi.

Awali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 TARURA katika bajeti yake wamepatiwa zaidi ya bilioni 10 fedha zilizotokana na tozo za mafuta ili zikasaidie katika ukarabati wa barabara katika Mkoa wa Arusha na kusaini Mikataba 52 yenye thamani ya bilioni 18 kwa ajili ya ukarabati wa barabara mbalimbali za Mkoa wa Arusha kwa mwaka wa fedha 2022/2023.





# RAS ARUSHA AMSHUKURU RAIS SAMIA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO

**Na Elinipa Lupembe**

Katibu Tawala mkoa wa Arusha, Misaille Musa, amemshukuru Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa fedha nyingi za utekelezaji wa miradi, miradi ambayo inaendelea kupunguza changamoto za upatikanaiji wa huduma kwa wananchi hususani waishio vijijini.

Katibu Tawala huyo, amesema hayo wakati wa ziara yake ya kikazi ya kukagua shughuli za utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.4 katika sekta ya afya, elimu na maendeleo ya jamii, halmashauri ya Arusha.

Ametoa shukrani hizo huku akiwapongeza watumishi na wananchi wa halmashauri hiyo kwa kushirikiana katika usimamizi wa miradi hiyo yenye ubora unaoendana na thamani ya fedha zilizotolewa na serikali kwa kutumia Force akaunti.

"Tunamshukuru sana mama Samia, kwa kutoa fedha nyingi za miradi, miradi ambayo kiuhalisia inakwenda kuwahudumia wananchi wa maeneo ya pembezoni wenye uhitaji, kukamilika kwa upanuzi wa kituo cha Afya Mwandeti kutasaidia kuhudumia wagonjwa pamoja na kuondoa vifo vya kina mama wajawazito na watoto".Amesisitiza Missaile.

Hata hivyo ameuagiza uongozi wa halmashauri ya Arusha, kwa kutumia fedha za mapato ya ndani kukamilisha maeneo madogo madogo yaliyosalia katika kukamilisha ujenzi jengo la mama na mtoto Mwandeti, ili na wananchi waanze kupata huduma kituoni hapo kabla ya mwisho wa mwaka huu.



Aidha miradi mingine inayotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa kituo cha afya Oloirieni milioni 450 za mapato ya ndani na upanuzi wa kituo cha Afya Mwandeti kwa shilingi milioni 590 kutoka serikali kuu ikiwa ni fedha za Uviko 19, tozo pamoja na wahisani.

Katika ziara hiyo, jumla ya miradi minne ikiwemo miradi iliyotekelezwa na TASAF ya Kivuko cha Moivo shilingi milioni 67 .1 na ujenzi wa mabweni mawili shule ya sekondari Oldonyowas kwa shilingi milioni 356 imetembelewa.




# WADAU KUTOKA UJERUMANI WAUNGA MKONO JUHUDI ZA SERIKALI

**Na Elinipa Lupembe**

Wadau wa Maendeleo halmashauri ya Arusha, kutoka nchini Ujerumani, wameendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kuboresha miundombinu ya Afya, lengo likiwa ni kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya kwa jamii, hususani maeneo ya vijijini.

Wadau wa shirika la Help for Maasai Children kwa ufadhili wa marafiki kutoka nchini Ujerumani, wamefanikisha mkakati huo wa serikali kwa kujenga nyumba ya mtumishi wa afya, yenye thamani ya shilingi milioni 30, kwenye zahanati ya Nameloki kijiji cha Losinoni juu Kata ya Oldongowas.

Akizungumza wakati wa kukabidhi nyumba hiyo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Arusha, mwakilishi wa marafiki hao kutoka Ujerumani, Andreas Reinke, amesema kuwa, wamefikia hatua hiyo kwa kuona adha ya upatikanaji wa matibabu kwa wananchi wa Losinoni juu, na kuamua kujenga zahanati na sasa kujenga nyumba ya mtumishi ili wananchi wapate huduma za dharura hasa nyakati za usiku.

"Tulijenga zahanati, tukaona tujenge nyumba ya mtumishi, ili kuongeza wigo wa upatikanaji huduma za afya kwa wepesi kwa wananchi wa Losinoni, tunaungana na Serikali ya Tanzania, kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya unaimarika kwa wananchi wote". Amesema Andreas.

Naye Mkurugenzi Mtendaji halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, licha ya kuwashukuru wadau hao amekiri kuthamini mchango huo mkubwa kwa wananchi, sambamba na kutekeleza vipaumbele vya Serikali ikiwemo kusogeza huduma za afya kwa wanachi kwa lengo la kupunguza vifo vya wanawake na watoto nchini.

Aidha Mkurugenzi Msumi amewataka wananchi wa Losinoni Juu, kuutunza mradi huo pamoja na wahudumu wa afya waliopangiwa kufanya kazi hapo, ili udumu kwa sasa na vizazi vijavyo.

"Wananchi wa Losinoni Juu, mmepata zahanati, serikali imeleta madaktari hapa, hakikisheni mnatunza miundombinu na mali zote pamoja na kushirikiana na watumishi hawa, ni ndugu zenu, ni watanzania wenzetu". Amesistiza Mkurugenzi Msumi

Hata hivyo wananchi wa Losinoni juu wamekiri kufurahishwa na uwepo wa zahanati na nyumba ya daktari, kwa kuwa imewarahishishia upatikanaji wa huduma pindi wanapokuwa wagonjwa lakini zaidi kwa kina mama wajawazito na watoto.

Naishiye Lomutiye amebainisha kuwa wajawazito waliteseka sana na kulazimika kujifungulia nyumbani, jambo ambalo ilikuwa ni hatari kwa maisha ya mama na mtoto, kwa sasa huduma kwa wajawazito zinapatikana hapa.

Naye Diwani wa kata ya Oldonyowas, Mhe. Kijana licha ya kuwashukuru marafiki hao, ameipongeza Serikali kwa kutoa wahudumu wa afya pamoja na vifaa tiba, vilivyofanikisha utoaji na upatikanaji wa matibabu kwa wananchi.

"Zahanati ilijengwa mwaka 2018, kwa juhudi za Serikali mwaka huu tumepata daktari na wauguzi, Serikali ya mama Samia inatuthamini sana, wananchi tuendelee kushirikiana na Serikali kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu". Ameweka wazi Mhe. Kijana.



# SIMAMIENI MIRADI YA BOOST KWA KUZINGATIA TARATIBU: WAZIRI OR-TAMISEMI

**Na Elinipa Lupembe**

Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Mhe.Angellah Kairuki amewataka wataalamu kusimamia utekelezaji wa miradi ya kuboresha na kuimarisha elimu ya Awali na Msingi (BOOST) kwa kufuata Miongozo, Sheria na Kanuni na taratibu zilizoainishwa.

Mhe. Waziri, ametoa wito huo wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo watalamu wa fani mtambuka kutoka ngazi ya Halmshauri na mikoa ya kanda ya Kaskazini, mafunzo yaliyofanyika kwenye shule ya Sekondari Ilboru wilaya ya Arumeru mkoa wa Arusha.

Mhe. Kairuki amewataka watalamu kutumia ujuzi na maarifa watakayoyapata kupitia mafunzi hayo kwenda kusimamia utekelezaji wa mradi wa BOOST katika maeneo yao ili kufikia malengo ya serikali ya mpango wa shule salama, zitakazomuwezsha mwanafunzi kuwa mahizi bila vikwazo.

"Kila halmashauri hakikisheni mnaelewa na kufuata afua zote za utekelezaji wa mradi kwa kuzingatia kanuni na taratibu, utunzaji wa nyaraka na uandaaji wa taarifa za mradi, tukamilishe miradi bila kuwa na hoja za ukaguzi" Amesisitiza Mhe. Waziri.

Aidha Waziri Kairuki, amebainisha lengo la serikali kupitia mradi wa BOOST ni kuwa na mpango salama wa shule, wenye mazingira rafiki yenye kupunguza vikwazo vya upatikanaji wa elimu kwa watoto pamoja na kuwajengea wanafunzi umahiri katika nyanja mbalimbali.

Hata hivyo Mhe. Waziri amewaonya wasimamizi wa utekelezaji wa mradi wa BOOST kuwa makini kwa kuepuka udanganyifu na ubadhilifu wa fedha hizo na kuweka wazi kuwa hatua kali zitachukuliwa dhidi ya watakaokwenda kinyume na taratibu zilizoelekezwa na serikali.

Naye Naibu Katibu Mkuu OR - TAMISEMI, Ramadhani Kairima amesema kwa kanda ya Kaskazini jumla ya wanafunzi wakufunzi 274 watajengewa uwezo wa mradi huo kutoka mikoa ya Arusha, Manyara na Singida na kusisitiza kuwa utekelezaji wa miradi ya BOOST kuwa agenda ya kudumu katika vikao vya kisheria vya halmashauri zote.

Aidha ameeleza lengo la mafunzo hayo ni kuzijengea uwezo timu za utekelezaji wa mradi wa BOOST ili kuwa na uelewa wa pamoja, na kuwawezesha kufahamu vema mradi wa BOOST, malengo ya mradi, hatua za utekelezaji na namna bora ya utekelezaji unaozingatia kanuni, aheria na taraibu kwa kuzingatia matokeo chanya yanayotarajiwa na serikalia.

Mradi BOOST umezinduliwa rasmi katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini na unategemea kutekelezwa ka kipindi cha miaka mitano kuanzi mwaka wa fedha 2022/2023 - 2025/2026, unaotegemea kujenga jumla ya madarasa 12,000 kwa gharama ya shilingi trilioni 1.15 sambamba na kuimarisha matumizi ya TEHAMA shuleni, lengo kuu likiwa ni kuboresha elimu ya awali na msingi.



# SERIKALI YAWAHAKIKISHIA WANAFUNZI 7, 857 KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2023

**Na Elinipa Lupembe**

Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imewahakikishia wanafunzi 7,856 waliofaulu mtihani wa darasa la saba mwaka 2022 sawa na asilimia 100, wamepangiwa shule za sekondari za serikali halmashauri ya Arusha.

Uthibitisho huo umetolewa na Mkuu wa wilaya ya Arumeru, Mhandisi Richard Ruyango wakati wa hafla ya makabidhiano ya mradi wa ujenzi wa vyumba 38 vya madarasa, vilivyojengwa maalum kwa ajili ya kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza Januari 2023.

Mkuu huyo wa wilaya amesema kuwa, kutokana na uwepo wa vyumba vya madarasa 134, ambavyo Serikali imewekeza kwa miaka miwili mfululizo vitawezesha idadi hiyo ya wanafunzi kuanza masomo yao mapema Januari 9.

"Mwishoni mwa mwaka 2021 tulipokea shilingi bilioni 2 na kujenga vyumba 96 vya madarasa na mwaka huu tumepokea milioni 769 na kujenga vyumba 38 kwenye shule 18 zilizokuwa na upungufu, madarasa hayo yatatumika kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza 2023". Ameweka wazi Mhandisi Ruyango.

Hata hivyo amewataka viongozi wote kusimamia na kuhakikisha wanafunzi wote waliopangiwa kujiunga na elimu hiyo ya sekondari, wanaanza masomo ifikapo tarehe 9 Januri 2023 na kuwaasa wazazi kuwapatia mahitaji yao ya msingi ya shule kama ilivyo kwenye fomu za kujiunga na shule hizo.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha, Mhe. Ojungu Salekwa amethibitisha kuwa, Serikali imeshafanya kazi yake, kazi iliyobaki ni kuhakikisha wanafunzi wote waliopangiwa kujiunga na kidato cha kwanza wanakwenda shule kwa wakati na kwa idadi kamili ya wanafunzi waliochaguliwa.

"Mama Samia ameshafanya kazi yake, kazi yetu ni moja kuhakikisha wanafunzi wote waliopangiwa kujiunga na kidato cha kwanza wanaanza shule kwa wakati, na wazazi kuhakikisha wanawapa watoto wao mahitaji yote ya shule". Amesema Mhe. Ojung'u.

Joshua Augustino ni mwanafunzi anayeingia Kidato cha pili shule ya sekondari Mringa licha ya kuishukuru Serikali kwa kuwajengea madarasa mazuri, ameahidi kusoma kwa bidii ili kufikia malengo yake na kuja kulitumikia Taifa lake la Tanzania.

Mwenyekiti wa Bodi ya shule ya sekondari Mringa Mwl. Jackson Mollel amesema kazi iliyofanywa na Serikali ni kubwa na inathamani kwa watoto na vizazi vyao, kazi ambayo imewapunguzia wananchi mzigo wa kuchangia ujenzi wa madarasa, michango ambayo ilikiwa inasuasua na kushindwa hata kukamilisha darasa moja kwa wakati.

Akiwasilisha taarifa ya mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji halmasahuri ya Arusha, Seleman Msumi, amesema kuwa halmashauri ilipokea shilingi milioni 760 na kujenga vyumba 38 vya madarasa, viti na meza 50 kwa kila darasa pamoja na ofisi 7 za walimu kwenye shule 6 kati ya shule 18 za sekondari.

Ifahamike kuwa ujenzi wa vyumba vya madarasa ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi Ibara ya 79 kifungu (q) Kukarabati miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika shule za Msingi na Sekondari nchini.




# MIAKA 61 YA UHURU WATANZANIA WATHIBITISHA MAFANIKIO MAKUBWA SEKTA YA ELIMU, UCHUMI NA AFYA

**Na Elinipa Lupembe**

Kuelekea maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika, wananchi halmashauri ya Arusha wilaya ya Arumeru wamekiri kuwepo mafanikio makubwa nchini katika sekta za elimu, uchumi na afya, yaliyotokana na juhudi za serikali za mapambano dhidi ya maadui ujinga, umaskini na maradhi.

Wananchi hao wamedhibitisha hayo, wakati wa Mdahalo maalum uliowashirikisha wakazi wa halmashauri ya Arusha, uliobeba mada ya "Miaka 61 ya Uhuru na Mapambano dhidi ya maadui Ujinga, Umaskini na Maradhi".

Mdahalo huo uliongozwa na Katibu Tawala Wilaya ya Arumeru Mwl. James Mchembe, wananchi wamebainisha matokeo ya mapambano dhidi ya ujinga yanayojidhihirisha wazi, kutokana na ongezeko la wasomi lililotokana na uwepo wa shule na vyuo vya kati na vikuu katika mikoa yote nchini, uliotoa fursa ya kila mtanzania kupata elimu.

"Kwa sasa Serikali imetoa fursa kila mtanzania kuwa na haki ya kupata elimu, kuanzia elimu ya awali mpaka chuo kikuu, tofauti kabla ya Uhuru elimu ilitolewa kwa ubaguzi, kubwa zaidi uwepo wa shule za serikali kila kata, za mashirika na binafsi kwa ujumla zimepanua wigo wa wananchi kuondokana na ujinga" Mwl. Emanuel Mkonongo.

Ameongeza kuwa baada ya Uhuru serikali ilijikita kwa wananchi wake kufuata ujinga kwa kuhakikisha wananchi wanajifunza Kusoma, Kuandika na kuhesabu, kwa sasa Taifa linatafuta wasomi wataalam wa fani mbalimbali na si wasomo wa KKK tatu.

Bw. James Magumba amezungumzia hali halisi ya mabadiliko katika sekta ya usafiri na usafirishaji, watanzania wakiwa wanajivunia maendeleo ya miundombinu ya barabara zinazofikika katika mikoa yote Tanzania hadi katika maeneo ya vijijini.

"Kwa sasa watanzania tunasafiri kutoka eneo moja kwenda jingine kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi, bila ya kuwa na kikwazo, tofauti kubwa baada ya Uhuru mtu alisafiri zaidi ya siku 4 sehemu ya kufika kwa siku moja, Mungu ibariki Tanzania" Amebainisha Bw. Magumba

Victo Karia amezungumzia mabadiliko katika sekta ya afya kuanzia mtu binafsi, upatikanaji wa huduma za afya, uwezeshwaji wa upatatikanaji wa huduma za afya pamoja na ushirikishwaji wa jamii katika kupambana na magonjwa kupitia watoa huduma ngazi ya jamii.

Bw. Karia amebainisha mabadiliko ya kiafya yaliyotokana na mapambano dhidi ya ujinga na umaskini yaliyomuwezesha mtanzania mwenyewe kufahamu namna ya kujikinga na maradhi kupitia lishe bora na usafi wa mtu na mazingira, jambo ambalo zamani watu wengi walipoteza maisha kutokana na magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu, surua, utapiamlo magonjwa ambayo watanzania wa sasa wamefahamu namna ya kujikinga.

Serikali imefanikiwa kuboresha sekta ya afya kwa kusogeza huduma za afya, karibu na wananchi kwa kuhakikusha kila kijiji kina zahanati, kata ina kituo cha afya, hosptali ya wilaya na kuwa hosptali za rufaa za mkoa, jambo ambalo licha ya kurahisisha upatikanaji wa matibabu, limeondoa msongamano hospitalini.

Mdahalo ni maalum kuelekea maadhimisho ya sikuu ya Uhuru wa Tanganyika tarehe 09.12.2022.uliofanyika kwenye ukumbi wa mikutano shule ya Msingi Green Acres.



# MB. ARUMERU MAGHARIBI: AWAMU YA SITA IMEPATA FEDHA NYINGI ZA MIRADI YA MAENDELEO

**Na Elinipa Lupembe**

Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi, Mhe. Noah Lembris amesema kuwa katika kipindi cha awamu ya sita, Jimbo lake limepata fedha nyingi za kutekeleza miradi ya maendeleo tofauti na awamu zilizotangulia.

Mhe. Noah ameyasema hayo wakati akitoa salamu kwa wananchi waliohudhuria hafla fupi ya makabidhiano ya mradi wa ujenzi wa vyumba 38 vya madarasa halmashauri ya Arusha, hafla iliyofanyika kwenye viwanja vya shule ya Sekondari Mringa.

Mbunge huyo ameeleza mafanikio ya Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambapo Jimbo hilo la Arumeru Magharibi limepata fedha nyingi za kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta za Elimu, Afya, maji na miundombinu ya barabara, miradi ambayo imeondoa kero zilizokuwa zikiwakabili wananchi wa jimbo hilo kwa muda mrefu.

Amesema kuwa licha ya kuwa mwaka 2022 Serikali imetoa shilingi Milioni 760 za kujenga madarasa 38 kwa ajili ya kuwapokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2023, amebainisha kuwa fedha hizo ni sehemu ndogo ya fedha ambazo Serikali ya awamu ya sita imezitoa jimboni humo.

"Milioni 760 ni sehemu tuu ya miradi iliyotekelezwa na Serikali ya CCM ndani ya Jimbo hili, lakini Serikali imetoa shilingi Bilioni 22 za ujenzi wa barabara yenye urefu wa Km 18 ya kutoka Mianzini, Timbolo, Sambasha mpaka Ngaramtoni, yote hayo ni mafanikio makubwa ndani ya Jimbo letu la Arumeru Magharibi kwa muda mfupi sana". Ameweka wazi Mhe. Noah.

Ameongeza kuwa wananchi wa Arumeru Magharibi wana kila sababu ya kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa miradi mingi ya maendeleo ambayo inatatua kero na changamoto nyingi katika hizo sambamba na kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi.

Aidha hakusita kuwapongeza watendaji wote kuanzia ngazi ya wilaya, halmashauri na kata na shule kwa kuhakikisha miradi yote inatekelezwa kwa ubora kwa kuzingatia viwango vinavyoendana na thamani ya fedha zilizotolewa na Serikali "value for money".





# FEDHA ZA UVIKO 19 KUENDELEZA KUKAMILISHA MRADI WA MAJI LESIRAA

**Na Elinipa Lupembe**

Kaimu Meneja wa RUWASA Wilaya ya Arumeru, Peter Maina, amesema kuwa Serikali inaendelea kutoa fedha za upanuzi wa miradi ya maji ambayo imeanza ili kufikia maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma ya maji.

Maji yamefika kijiji cha Lesiraa lakini kuna baadhi ya maeneo hayajafika hususani kitongoji cha Bwawani, kadri fedha zitakavyotolewa na Serikali mradi huo utapanuliwa ili kuwafikia wananchi wa kitongoji hicho cha Bwawani.

Maina ametoa ufafanuzi huo wakati akijibu swali lilioulizwa na Diwani wa Kata ya Kisongo aliyeomba ufafanuzi wa hatima ya mradi wa maji Lesira kwa kuwafikia wanachi wa kitongoji cha Bwawani kilichopo ndani ya kijiji hicho, wakati wa mkutano wa Baraza la Madiwani wa Taarifa za robo ya Julai - Septemba 2022.

Hata hiyo Maina amesema kuwa Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya ukamilishaji na upanuzi wa miradi ya maji ambayo imeanza ili kufikia maeneo ambayo hayajapata huduma za maji.

Akiwasilisha taarifa yake Kaimu Meneja huyo amebainisha kuwa, katika kipindi cha robo ya kwanza RUWASA imendelea kutekeleza miradi ya maji kupitia fedha za Mfuko wa Maji (NWF), Fedha za UVIKO 19 na fedha za malipo kwa matokeo (PbRV).



Aidha amefafanua kiasi cha shilingi milioni 801.1 za NWF, zinatekeleza mradi wa maji Losikito kukiwa na ujenzi wa nyumba ya pampu, tanki la kukusanyia maji na uzio, huku milioni 376 za PbRV zikitekeleza mradi wa maji Manyire, Marurani na Majimoto shilingi milioni 200 na mradi wa maji Old Nduruma kwa shilingi milioni 176 na yote imefikia asilimia 90 ya utekelazaji wake.



# TASAF YAWAHAKIKISHIA HEDHI SALAMA WASICHANA WA KAYA MASIKINI

**Na Elinipa Lupembe**

Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwa ufadhili wa shirika la watoto Duniani (UNICEF) wametoa vifaa vya kujisitiri wakati wa hedhi kwa wasichana 12,943 wanaotoka kwenye kaya zilizo kwenye mpango wa kunusuru kaya masikini.

Akizungumza wakati wa kukabidhi taulo hizo, kwa wasichana wa Kata ya Kiutu, Mkurugenzi Mtendaji halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi ameishukuru Serikali kupitia TASAF kwa kutoa vifaa hivyo ikiwemo taulo za kike, vifaa ambavyo vinawahakikishia watoto kuwa na hedhi salama isiyo na vikwazo.

Ameongeza kuwa vifaa hivi ni mkakati wa Serikali wa kuhakikisha mazingira bora ya wanafunzi kupata elimu bila kikwazo na kuhakikisha watoto wote wanahudhuria masomo pasi kuwa na tatizo la kiafya hususani kipindi cha hedhi.

"Serikali inahakikisha kila mwanafunzi anahudhuria masomo mwaka mzima, bila kuwa na vikwazo, hivyo tunzeni vifaa hivyo, kwa kuhakikisha vinawasidia muda wote wa hedhi.

Hata hivyo wanafunzi hao, wamemshukuru mheshimwa Rais Dkt. Samia Suluhu kupitia TASAF kwa msaada huo, ambao wamebainisha kuwa ni kuwafanya watoto wa kaya masikini kupata mahitaji sawa na watoto wengine.

Catherini Felix msichana aliyehitimu kidato cha IV mwaka huu 2022 shule ya sekondari Sokoni II amesema kuwa baadhi ya wazazi wamekuwa wakishindwa kumudu kuwanunulia watoto wao wa kike vifaa



salama wakati wa hedhi kutokana na uwezo wa kifedha kuwa mdogo, lakini Serikali imekuja kuwasaidia wasichana wengi kutoka famili zisizo na uwezo mkubwa kifedha.

Baadhi ya wasichana hushindwa kuja shuleni wakati wa hedhi kutokana na kukosa taulo za kike, na kuwafanya kushindwa kufanya vizuri kitaaluma sawa na wavulana." Amefafanua Lightnes Maina msichana aliyehitimu kidato cha IV mwaka huu Sekondari Sokon II.

Awali Mratibu wa TASAF Halmashauri ya Arusha, Grace Makema, amethitisha kupokea vifaa vya wasichana 12, 943 kwa ajili ya wasichana walio kwenye kaya 12, 288 zinazonufaika na Mpango wa Kunusuru kaya Maskini kwenye vijiji 88 vya halmasahuri hiyo.

Ifahamike kuwa Miradi ya Serikali inayotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika kusimamia Serikali kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika kukabiliana na changamoto za umasikini kwa wananchi nchini.



# WANUFAIKA WA MIKOPO WATAKIWA KUFANYA MIRADI ITAKAYOWAWEZESHA KUFANYA MAREJESHO

**Na Mwandishi wetu**

Wanufaika wa mikopo isiyo na riba ya asilimia 10 ya mapato ya ndani inayotolewa na halmashauri kwa vikundi vya vijana, kina mama na walemavu, wametakiwa kufanya shughuli za uzalishaji zenye tija na zitakazoleta faida ili kupata faida na kumudu kurejesha mikopo hiyo.

Rai hiyo imetolewa na Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Arusha, Angela Mvaa wakati walipokutana na wanavikundi hao kwaajili ya kusaini, mikataba ya kupokea fedha hizo, fedha ambazo zitarejesha kwa kipindi cha mwaka mmoja, katika ukumbi wa mikutano wa halmashauri hiyo.

Afisa Maendeleo huyo amebainisha kuwa ni vema kila kikundi kujikita kwenye shughuli za mradi ambao mmewasilisha kwenye andiko na kusimamia mradi huo ili uweze kuleta faida kwa manufaa ya familia na kurejesha deni pia.

Aidha amesema kuwa, ni muhimu kila mwanakikundi kutambua masharti ya mkopo unaotolewa na Serikali ya Awamu ya sita na kuwajibika ipasavyo kufanya shughuli za miradi iliyokusudiwa ili fedha hizo ziweze kurudishwa kwa wakati na kusisitiza utunzaji wa kumbukumbu za matumizi yote ya fedha ili kuepuka upotevu wa fedha za Serikali.

"Mikopo hii inatolewa kwa watu waliokidhi vigezo kulingana na kiasi cha fedha kilichopo na si vinginevyo, ninyi mna sifa na mmekidhi vigezo vya kupata mkopo huu, niwaombe kuepuka matumizi yoyote yasiyo ya lazima ili muweze kufikia malengo yenu na kurejesha fedha hizo kwa wakati." Alisisitiza Mvaa.

Naye Afisa Maendeleo ya Jamii dawati la vijana halmashauri ya Arusha, Ahadi Mlay amesema kuwa lengo la Serikali kutoa mikopo hiyo isiyo na ribariba, walemavu, vikundi vya vijana na akinamama ni kutoa fursa kwa jamii kuinuka kiuchumi kupitia shughuli mbalimbli za uzalishaji ikiwa ni pamoja na kuzakuza ajira hasa kwa vijana ambao wanapitia changamoto ya kukosa mitaji ya kuanzisha biashara.

"Fedha hizi sio kwa ajili ya kugawana kwa kila mwanakikundi na kila mtu kufanya mradi anaotaka bali ni kwaajili ya kufanya mradi uliokusudiwa na wanakikundi wote kwa pamoja na faida itakayopatikana ndiyo inapaswa kugawanywa kwa kila mwanakundi." Ameweka wazi Mlay.

Hata hivyo wanufaika hao wameishukuru Serikali ya Awamu ya sita, inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwajali, wananchi wake na kuwapatia fursa nyingi za kujikwamua kiuchumi pamoja na kuzalisha ajira kwa watanzania waliokuwa wamekata tamaa ya kujiendeleza, kiuchumi kutokana na kukosa mitaji ya kufanyia biashara.

"Matamanio yangu ni kukuza biashara yangu ya nafaka, matunda na mbogamboga na kuwekeza zaidi ili niweze kuwa mfanyabiashara mkubwa, ninaishukuru sana Serikali kwa kutupatia fursa hii addhimu na ninawashauri na watanzania wengine kuchangamkia fursa hii masharti yake siyo magumu na hakuna ubaguzi." Alisema Michael Thomas ambaye ni mlemavu wa Kata ya Mateves, mara baada ya kusaini mkataba wa mkopo

Awali, halmashauri ya Arusha imetoa shilingi milioni 217.6 kwa vikundi 15 ambapo, fedha hizo zinatarajiwa kurejeshwa kwa kipindi cha ndani ya miaka mitatu.




# WAZAZI KUSHINDWA KUWASIMAMIA WATOTO; CHANZO CHA ULAWITI KWA WATOTO WA KIUME

**Na Elinipa Lupembe**

Watoto wa kiume shule za msingi, wamebainisha kuwa chanzo kikubwa cha ulawiti kwa watoto wa kiume ni wazazi kushindwa kuwasimamia watoto wao katika malezi kwa kujikita zaidi kwenye mambo yao na kuwaacha watoto wakijilea wenyewe.

Watoto hao wametoa maoni hayo wakati wa midahalo ya kutoa elimu ya Ulawiti, iliyofanyika baina ya Kamati ya Kupinga Ukatili wa Ulawiti kwa wavulana 'Father on Duty' na klabu za Maabara za wavulana shuleni (Boy's Vac Lab), mdahalo uliofanyika kwenye shule 4 za msingi halmashauri ya Arusha.

Watoto wameelekeza malalamiko yao kwa wazazi kwa kueleza kuwa baadhi ya wazazi wamepoteza maadili kwa kufanya mambo mabaya mbele ya watoto na wengine kujikita zaidi kwenye kutafuta pesa za kuendesha maisha na kuwaacha watoto wakijilea wenyewe majumbani.

Hansa Masawe mwanafunzi (VI) shule ya msingi Ilboru, amebainisha kuwa baadhi ya wazazi na watu wazima hufanya vitendo vya ngono huku watoto wakiona jambo ambalo linawafanya watoto nao kuiga na kuanza kufanyiana wenyewe kwa wenyewe.

Lomnyaki Mollel mwanafunzi (V) shule ya msingi Olturoto amebainisha kuwa kwa sasa wazazi wanatumia muda mwingi kutafuta pesa za kuendesha maisha na kuwaacha watoto chini ya uangalizi wa ndugu, jamaa na marafiki, watu hao huanza kuwalawiti watoto na watoto huzoea na kuanza kufanyiana wenyewe kwa wenyewe.

Nasiri Shaban mwanafunzi wa shule ya msingi Naurei, ameeleza kuwa, tabia ya wazazi kuacha watoto wanalala na wageni wajapo nyumbani nayo ni chanzo cha ulawiti kwa watoto wa kiume, na kuwataka wazazi kuacha tabia ya kuwalaza wageni kwenye vyumba vya watoto.

Hata hivyo wanavulana hao wamelalamikia, kitendo cha jamii kuwatetea watoto wa kike na kuwaacha watoto wa kiume kando, kimesababisha wakatili kugeukia kwa watoto wa kiume, madhara yake yameanza kuonekana, hivyo jamii inapaswa kuelekeza nguvu pia kupambana na ukatili dhidi ya watoto wa kiume hususani kwenye vitendo vya ulawiti.

Mratibu wa Kuthibiti Maambukizi ya UKIMWI Halmashauri ya Arusha, Dkt. Japhet Champanda, ameeleza madhara ya watoto kulawitiwa kiafya ni pamoja na kushindwa kuzuia haja kubwa, kupata mamabukizi ya magonjwa ya zinaa ambayo yakiingia sehemu ya haja kubwa ni vigumu sana kutibika.

"Athari za ulawiti, humuondelea mwanaume urijali na kuathirika kisaikolojia kwa kushindwa kujiamini na kushindwa kutekeleza majukumu yake kama mwanaume." Amesisitiza Dkt. Champanda.

Hata hivyo wajumbe wa kamati ya Father on Duty wamewataka watoto kukataa kuingiliwa na wanaume wenzao na kutoa taarifa pale wanapohisi mtu mwenye nia ovu ya kuwafanyia vitendo hivyo, pamoja kutoa taarifa za siri kwa walimu kama kuna watoto wanafanyiana vitendo hivyo.

Halmashauri ya Arusha kwa kushirikiana na shirika la CWCD, linatekeleza mradi wa kupinga ukatili wa kingono na ulawiti kwa watoto wa kiume, kupitia maabara za wavulana "Boy's Vac Lab" katika shule za msingi za Naurei, Moivo, Ilboru, Olturoto, Kiranyi na Ngaramtono kwa ufathili wa Foundation for Civil Society.



# WAZAZI WATAKIWA KUPAMBANA NA UKATILI WA KINGONO KWA WATOTO WA KIUME

**Na Elinipa Lupembe**

Wazazi na walezi wametakiwa kuamka na kuanza harakati madhubuti za kupambana na ukatili wa kingono dhidi ya watoto wa kiume, kama inavyofanyika kwa watoto wa kike kwa kipindi kirefu sasa.

Rai hiyo imetolewa na Afisa Maendeleo ya Jamii, Dawati la Jinsia, Rovil Nguyaine, wakati wa kikao kazi kilichojumuisha wajumbe wa Kamati ya MTAKUWWA ngazi ya Kata kutoka Kata 6 za halmashauri ya Arusha, kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa halmashauri hiyo.

Nguyaine amebainisha ongezeko la kasi la matukio ya ulawiti kwa watoto wa kiume, watoto ambao wazazi na jamii hawakushughulika nao kwa dhana ya kuwa wanao uwezo wa kujitetea kiume, jambo ambalo madhara yake yameanza kuonekana sasa.

Ameongeza kuwa ni jukumu la wazazi na jamii, kuhakikisha wanawalinda watoto wote dhidi ya ukatili wa kijinsia na sio watoto wa kike peke yao, kwa kuwa watoto wote ni sawa na wanahitaji kulindwa kuanzia nyumbani, njiani mpaka shuleni.

"Wazazi/ Walezi jengeni desturi ya kushirikiana na walimu katika kupambana na ukatili wa kijinsia, hakikisheni mnakuwa karibu na watoto wenu, kwa kuwa hali ya ukatili ni mbaya sana hasa kwa wtoto wa kiume." Amesema Nguyaine.

Hata hivyo wajumbe hao wa kamati ya MTAKUWWA licha ya kushukuru kikao kazi hicho, wamethibitisha uwepo wa matukio ya ukatili kwa watoto wa kiume na kuahidi kuendelea kuhamasisha jamii kujikita kupambana na ukatili kwa watoto wote wa kike na wa kiume.

Wameongeza kuwa, kupitia mafunzo wanayopewa na Serikali na mashirika juu ya ulinzi na usalama wa watoto, umewezesha jamii kuanza kuwa na uelewa wa pamoja juu ya usimamizi wa usalama na haki za watoto.

Naye mjumbe wa Kamati ya MTAKUWWA kata ya Moivo Elizabeth, amelilalamikia jeshi la Polisi kuwa na vikwazo wakati wa ufuatiliaji wa kesi za ukatili na kuweka wazi kuwa, kutokana na ukiritimba uliopo, unasababisha wengi kurudi nyuma kwa kukata tamaa kutokana na usumbufu.

Hata hivyo Mratibu wa Dawati la Jinsia, na Mpelezi wa kesi za Ukatili, Kituo cha Polisi Ngaramtoni, Koplo Jane Mandi amewataka wazazi na wajumbe wa MTAKUWWA kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa matukio yoyote ya ukatili pamoja nakufuata taratibu ambazo zitawezesha kesi kufika mwisho na hatimaye watoto kupata haki zao.

"Jeshi la Polisi liko tayari kushirikiana na kamati za MTAKUWWA kwa matukio yote ya ukatili na kuhakikisha watuhumiwa wanatiwa hatiani na kujitoa kutoa ushahidi kwenye kesi ili watoto waweze kupata haki zao, kwa sasa Jeshi la Polisi linasimamia kwa uwazi haki za watoto."

Koplo Jane amezungumzia mila na desturi za jamii bado ni kikwazo cha kesi nyingi za ukatili kutokana na ukweli kwamba matukio hayo yanatokea ndani ya familia na kusababisha wahanga kuogopa kutengwa na familia zao.

Awali Mratibu wa Mradi wa Kupinga Ukatili wa Kingono dhidi ya Watoto wa kiume, Shirika la CWCD, Mariam Rashid amesema kuwa lengo la kikao kazi hicho ni kukumbushana majukumu kwa wajumbe wa kamati ya MTAKUWWA na kuwashirikisha kushiriki mradi wa ukatili wa kingono kwa wavulana unaonedelea kwenye kata zao.

Halmashauri ya Arusha kwa kushirikiana na shirika la Center for Women and Children Develepment ( CWCD), wanatekeleza mradi wa kupinga ukatili wa kingono kwa watoto wa kiume kwenye kata 6, kwa ufadhili wa Foundation for Civil Society.



# DC ARUMERU AWASISITIZA MADIWANI KUIMARISHA MIKAKATI YA UKUSANYAJI WA MAPATO

**Na Elinipa Lupembe**

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Mhandisi Richard Ruyango, ametoa salamu kwa wajumbe wa baraza la Madiwani kwa kuushukuru na kuupongeza uongozi wa halmashauri ya Arusha kwa juhudi kubwa zinazofanyika katika kuwahudumia wananchi na kuwasisitiza kuimarisha mikakati ya ukusanyaji wa Mapato.

Akizungumza baada ya ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Madiwani la kujadili taarifa za robo ya kwanza Julai -Septemba 2022, Mkuu huyo wa Wilaya, amewahimiza waheshimiwa Madiwani licha ya juhudi zinazofanyika suala la ukusanyaji wa mapato ni la muhimu zaidi pamoja na kubuni vyanzo vipya vya mapato.

Mkuu huyo wa wilaya ameweka wazi kuwa, ili halmashauri iweze kutimiza mipango na malengo yake, ni lazima ukusanyaji wa mapato ufanyike kwa ufanisi kulingana na makisio ya kibajeti pamoja na kusimamia matumizi ya mapato hayo.

Aidha mhandisi Ruyango, amesisitiza matumizi ya makusanyo yanayozingatia sheria na maelekezo ya Serikali ikiwemo asilimia 10 kwa ajili ya mikopo isiyokuwa na riba kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kama maelekezo ya Serikali yanavyoelekeza.

Hata hivyo, mkuu wa wilaya amemsisitiza Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, kusimamia makusanyo ya mapato hasa kwa mapato yanayokusanywa kwa mashine za POS kuweka fedha hizo benki kama sheria inavyoelekeza ya kuwasilisha fedha zote benki mara baada ya kuzikusanya.

Awali amewakumbusha waheshimiwa madiwani, kushiriki katika usimamizi wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao, pamoja na kuwashirikisha wananchi katika usimamizi wa miradi hiyo.

"Halmashauri imepokea fedha kutoka Serikali Kuu, shilingi milioni 760 za ujenzi wa vyumba 38 vya madarasa kwa shule 18 za sekondari kwa ajili ya kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka wa masomo 2023, hivyo kila aliyepewa dhamana ahakikishe anashiriki kikamilifu kusimamia miradi hiyo kwa mujibu wa sheria." Amesisitiza Mkuu wa wilaya .

Aidha amaemuagiza Mkurugenzi wa halmashauri kutoa taarifa kwa viongozi wa ngazi zote ikiwemo Madiwani, za miradi yote inayokwenda kutekelezwa kwenye maeneo yao ya kata, vijiji na vitongoji, ili viongozi wote washiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Waheshimiwa Madiwani, mnatakiwa kufanya mipango ya kuhamasisha wanafunzi wanapata chakula cha mchana wawapo shuleni na kuwahasisha wazazi kuchangia changia chakula cha mchana kwa shule za kutwa.





# ASAS YA AAIDRO YAZINDUA MRADI WA MILIONI 230 KUWAINUA WANANCHI KIUCHUMI

**Na Elinipa Lupembe**

ASAS ya Kiraia ya AAIDRO ya kanisa Katoliki Jimbo Kuu Arusha chini ya Idara ya Jinsia na Wanawake imezindua mradi wa kuwainua wananchi wenye hali ya chini kiuchumu katika kata za Nduruma na Bwawani Halmashauri ya Arusha.

Akizungumza wakati wa kuutambulisha mradi huo, kwenye ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji halmashauri ya Arusha, kwa niaba ya Kanisa Katoliki Padri Faustine Moshi, amesema kuwa mradi huo utatekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja na utahusisha makundi rika tofauti kwa lengo la kuwawezesha wananchi kijiinua kiuchumi na kijamii.

Aidha Padri Mosha amesema kuwa Kanisa limeona ni vema kushirikiana na Serikali kuwahudumia wananchi katika sekta nyingine zaidi ya ile ya kiroho, na kuongeza kuwa wanatarajia kupata ushirikiano mkubwa kutoka kwa watalamu wa halmashauri ili kufikia lengo la kanisa na malengo ya serikali ya kuwahudumia wananchi.

"Utekelezaji wa mradi huu utagharimu takribani shilingi milioni 230 na kuwajengea uwezo watu 200 kupitia vikundi, hivyo ni matumaini yetu, kazi hii itafanywa na kanisa na watalamu kutoka serikalini kupiti halmashauri, kwa pamoja tutafikia lengo".Amesisitiza Padri Mosha.

Hata hivyo Mkurugenzi Mtendaji halmashauri ya Arusha Seleman Msumi, amelishukuru Kanisa kupitia ASAS ya AAIDRO kwa kuona umuhimu wa kuunga mkono juhudi za serikali za kuwajengea uwezo wananchi kujikwamua kiuchumi, kazi ambayo ingefanywa na serikali.

"Kama Hamashauri tuko tayari kushirikiana na kanisa kwa kuzingatia jukumu la serikali ni kuweka mazingira rafiki kwa mashirika yanayofanya kazi za kuhudumia jamii kulingana na mpango mkakati wa serikali, tunao watalamu wa kutosha katika idara zote, hivyo watashirikiana nanyi katika hatua zote za utekelezaji wa mradi huu". Amesbainisha Mkurugenzi Msumi.

Aidha amelitaka shirika hilo Kwenda kutekeleza mradi huo kulinga na andiko la mradi na si vinginevyo, sambamba na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mradi huo kila robo ya mwaka kwenye vikao vya kisheria vya mashirika yasiyo ya kiserikali.

Naye mratibu wa mradi huo, Irene Moshi, amefananua kuwa mradi huo utajikita katika kuwapa mafunzo wakulima na kufanya kilimo cha kisasa, kilimo biashara kulingana na Ajenda 10/30, kuwajengea uwezo wajasiriamali pamoja na masuala mtambuka ya kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanaume, wanawake na watoto ikiwemo ukeketaji na ndoa za utotoni.

"Kupitia mradi huu tunategemea kuwaiwezesha jamii kuwa na uwezo wa kujikomboa kifkra, uwezo wa kujitegemea kiuchumi katika kujipatia pato la familia, pamoja na kuwa na jamii huru isiyokuwa na ukatili wa aina yoyote katika masuala ya kijinsia". Amesistiza Irene

Awali kwa sasa mradi huo uko katika hatua za awali, utatekelezwa kwa muda wa mwaka mmoja na unategemea kukamilika ifikapo Juni 2023.



# JAMII YATAKIWA KUACHA FIKRA POTOFU JUU CHANJO NA DAWA TIBA ZINAZOTOLEWA NA SERIKALI

**Na mwandishi wetu**

Jamii imetakiwa kuachana na dhana potofu za kudhani kuwa chanjo na kinga tiba zinazotolewa na serikali zina madhara kwa afya ya binadamu na kushawishi wengine kukataa.

Rai hiyo imetolewa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha, Mhe. Ojung'u Salekwa, wakati akizindua zoezi la kitaifa la umezeshaji vidonge vya kinga tiba dhidi ya minyoo tumbo kwa watoto wa umri wa miaka 5 mpaka 14 halmashauri ya Arusha, uzinduzi uliofanyika kwenye shule ya msingi Olgilai kata ya Kiutu.

Mhe. Ojung'u amesema kuwa chanjo na kinga tiba zinazotolewa na serikali zikiwa zimepimwa na kuthibitishwa kuwa na viwango vya ubora kwa binadamu zaidi ni salama kwa afya za binadamu.

"Serikali inathamini afya za watanzania, na inaweka mipango thabiti ya kuwakinga wananchi hususani watoto dhidi ya magonjwa ambayo yana kinga, kwa kuwa kinga ni bora kuliko tiba".Amesema Mhe. Mwenyekiti.

Katika zoezi hilo Diwani wa kata ya Kiutu, ameishukuru serikali kwa kutoa kinga tiba hiyo ambayo inawakinga watoto dhidi ya minyoo tumbo ambayo ina madhara makubwa kwa afya ya binadamu hususani watoto.

Mganga Mkuu halmashauri ya Arusha, Dkt. Petro Mboya, amesema kuwa vidonge vinavyotolewa ni almebendazole ambavyo hukinga dhidi ya minyoo tumbo na hutolewa kwa watoto kwa sababu wako kwenye hatari ya kupata mayai ya minyoo kutokana na tabia za michezo ya watoto.

"Tunatoa kinga tiba kwa watoto wa miaka 5 mpaka 14 kwa kuwa wako kwenye hatari ya kupatwa na mayai ya minyoo, kutokana na uwezo wao mdogo wa kujikinga na uchafu, watoto wengi hushindwa kunawa mikono na hula bila kunawa mikono na wakati mwingine huokota vitu na kula". Amebainisha Dkt. Mboya.

Mwalimu mkuu shule ya Msingi Oligilai, Mwl. Recho Kisiri, amesema kuwa, wanafunzi wamehudhuria masomo kwa wingi wao na wanategemea kumezesha dawa za minyoo takriban watoto 782 na kufikia asilimia 100.

Hata hivyo mratibu wa Magonjwa yasiyopewa Kipaumbele, Halmashauri ya Arusha, Ramadhani Kulewa, amesema kuwa, dawa tiba hiyo inatolewa kwenye vituo 211, shule za msingi 155, vituo vya afya 56, huku wahudumu 433 wakigawa dawa hiyo ambapo walimu ni 310 na wahudumu wa afya 112.

Awali Halmashauri inategemea kuwapatia kinga tiba ya minyoo kwa watoto elfu 80, watoto elfu 76 kati yao ni wale waliosajiliwa shuleni na watoto elfu 4 ni ambao hawajasajiliwa kwenye mfumo rasmi wa elimu.





# HATIMAYE KIJIJI CHA SAMARIA WAPATA NEEMA YA MAJI SAFI NA SALAMA

**Na mwandishi wetu**

Baada ya mateso ya muda mrefu ya changamoto ya upagikanaji wa maji, hatimaye wananchi wa kijiji cha Samaria kata ya Nduruma, Halmashauri ya Arusha, wamepata neema ya kupata maji safi na salama, baada ya serikali kutoa milioni 30 za kukamilika kwa mradi huo wa maji.

Wananchi hao waishukuru serikali kwa kusadia kutekeleza mradi wa maji ya kisima, ambao tayari umeanza kuwanufaisha wananchi hao na kusahau tabu waliyoipata kwa kipindi kirefu, kwa kutumia muda mrefu kutafuta maji, hali iliyosababisha kuzorota kwa baadhi ya shughuli nyingine za kijamii na kiuchumi.

Wakizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo, wananchi wamekiri, kukamilika kwa mradi kumekuwa na faida kubwa kwa kuwa, umeondoa adha iliyokuwepo hapo hususani kwa kina mama ambao waliteseka kutafuta maji.

"Sasa tumefikia ukomo wa mateso ya kutafuta maji, wanawake wa Samaria, tunaishukuru Serikali kwa kutushika mkono na kukamilisha mradi, upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama hasa umetuondolea kero kubwa kinama, tunaamini Serikali itaendelea kutusaidia ili maji yafike katika maeneo yote ya kijiji cha Samaria". Alisema Damari Nnko Mkazi wa Samaria.

Hata hivyo, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi Mhe. Noah Lembris, ameweka wazi kuwa lengo la Serikali ni kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma za muhimu ikiwemo maji safi na salama ndani ya mita 400 huku akiwataka viongozi wa maeneo hayo kusimamia kwa uadilifu mradi huo ili kila mwananchi aweze kunufaika.

"Tunajipanga vyema namna ya kupanua na kuendeleza mradi huu kwa kusogeza huduma ya maji karibu na wananchi, niwaombe wananchi wa tuendelee kuwa wazalendo kwa mradi huu ili uweze kudumu kwa muda mrefu, shirikianeni na viongozi wa Serikali ya kijiji kuhakikisha mradi unawanufaisha wananchi wote". Alisisitiza Mhe. Noah

Naye Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Arusha Seleman Msumi, ameishukuru familia iliyotoa eneo kwaajili ya kutekeleza mradi huo na kusisitiza kuwa kila mwananchi ana wajibu wa kutunza miundombinu iliyojengwa katika eneo hilo ili iendelee kuwasaidia wananduruma pamoja na vizazi vijavyo.

"Kwa kipindi kirefu kulikuwa na shida ya maji katika eneo hili, mama zetu walikuwa wanahangaika huku na kule kutafuta maji, mateso yalikuwa makubwa sana, lakini leo tunamshukuru Mungu kwa kukamilika kwa mradi huu, nawasihi kuendelea kutunza miundombinu hii ili iidumu na kuwahudumia wananchi wote". Amesema Mkurugenzi Msumi.

Aidha Diwani Kata ya Nduruma Mhe. Raymond Mollel, amesema kutokana na historia ya eneo hilo ilisemekana kuwa hakuna uwezekano wa kupata maji katika Kijiji hicho, hivyo uwepo wa kisima hicho ni neema kubwa kwa wakazi wa Samaria.

Mradi wa kisima cha maji ulianza kutekelezwa kwa nguvu za wananchi baadaye Halmashauri ilitoa kiasi cha Milioni 30 fedha za mapato ya ndani na kukamilisha mradi huo.



# KIVULINI MARTENITY AFRICA MKOMBOZI WA WAJAWAZITO

**Na Elinipa Lupembe**

Kituo cha afya cha Kivulini Martenity Afrika kimekuwa mkombozi wa wanawake wajawazito kwa kuwa kituo hicho ni kituo maalum cha kutoa huduma za kujifungua kwa kina mama wajawazito na matibabu ya wagonjwa wa fistula, kikifanikisha kupunguza vifo vya wanawake na watoto wakati wa kujifungua.

Kufuatia utoaji huduma hizo, Kivulini kimeongeza kujenga jengo la kupumzikia wajawazito wenye changamoto za uzazi na wale waliokaribia kujifungua kwa ajili ya kuwa na uangalizi wa karibu wa madaktari kwa mjazito, jengo lenye uwezo wa kupumzisha wajawazito 20, lililogharimu shilingi milioni 90.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa jengo hilo, Mkurugenzi Mkazi Maternity Africa. Michael Hynds, amesema kuwa, lengo la kuongeza jengo hilo ni kupata wodi ua wapumzisha wajawazito waliokaribia kujifungua na wale wenye changamoto ili kuwa karibu na uangalizi wa madaktari.

"Tumefikia hatua hii, kutokana na changamoto iliyokuwa ya kukosa mahali pa kuwapumzisha wajawazito, jambo ambalo awali lilihatarisha maisha ya kina mama na watoto, lakini kuwepo kwa jengo hili, kutaokoa maisha ya mama na mtoto" . Amesisitiza Hinds.

Hata hivyo mkurugenzi Mtendaji halmashauri ya Arusha, baada ya kuzindua jengo hilo, ameushukuru uongozi wa Kituo cha Maternity Afica kwa huduma bora za uzazi wanazozitoa kwa kina mama wa kitanzania, huduma ambazo zimesaidia kupunguza vifo vya mama na mtoto wakati wa kujifungua katika halmashauri.

Mkurigenzi Msumi ameongeza kuwa, serikali inathamini huduma ya kipekee inayotolewa na kituo cha Kivulini, kituo ambacho kinafanya kazi kubwa yenye baraka za kiMungu zilizopaswa kufanywa na serikali na kuridhishwa namna wagonjwa wanapatiwa huduma bure bila malipo yoyote.

Muuguzi Mkuu, halmashauri ya Arudha Noemi Themi, amesema, kituo hicho kimepunguza msongamano wa wajawazito kwenye vituo vya serikali kwa mkoa wa Arusha na mikoa jirani, hususani wale wenye changamoto za uzazi na ugonjwa wa fistula.

Nao wagonjwa waliolazwa kwenye kituo hicho cha afya, wameponheza na kushukuru huduma bora inayotolewa hapo bila malipo yoyote ikiwemo, matibabu, malazi ma chakula, jambo ambalo limeokoa maisha ya familia zisizo na uwezo.

Suzana Msami (26) mkazi wa Muleba mkoani Kagera, amethibitisha kutibiwa ugonjwa wa Vistula, ugonjwa ambao alihangaika nao kwa muda mrefu kwenye hospitali za Muleba na Bugando bila mafanikio

"Nilipataa rufaa kutoka hospitali ya Bugando, na nimetibiwa kwa sasa ninaendelea vizuri, sikuwa na pesa za matibabu, hapa nimetibiwa bure na kupatiwa huduma za chakula na malazi bure, ninamshukuru Mungu ninawashukuru madaktari na wauguzi kwa upendo uliorejesha furaha na matumaini ya maisha yangu tena" .Amesisitiza Suzana

Kituo cha Afya Maternity Africa kilifunguliwa mwaka 2018 na mpaka sasa jumla ya akinamama 8500 wamejifunguliwa kituoni hapo huku zaidi ya wagonjwa 550 wametibiwa ugonjwa wa Fistula na wanategemea sasa kuhudumia zaidi ya wagonjwa elfu tatu kwa mwaka.



# RC MONGELA AAGIZA: ZOEZI LA UBOMOAJI NYUMBA BARABARA YA MIANZINI - TIMBOLO, MWISHO DISEMBA 26, 2022

**Na Elinipa Lupembe**

Mkuu wa mkoa wa Arusha John Mongela ameagiza waliojenga nyumba ndani ya mita 10 za barabara ya Mianzini , Timbolo, Sambasha hadi Ngaramtoni, kubomoa nyumba zote hizo, kabla ya tarehe 26, Desemba 2022, ili kupisha ujenzi wa barabara unaoendelea.

Mkuu huyo wa mkao ametoa kauli hiyo alipotembela na kukagua maendeleo ya ujenzi wa barabara hiyo yenye urefu wa Km 18, inayojengwa kwa kiwango cha lami, mradi unaotekelezwa katika halmashauri za Jiji la Arusha na Arusha, utakaogharimu shilingi bilioni 22 hadi kukamilika kwake na kwa sasa ujenzi umefikia asilimia 8.

Mongella amefafanua kuwa kwa mujibu wa sheria ya barabara ya mwaka 2007 upana wa barabara ulitakiwa kuwa mita 20 kila upande, lakini serikali ya Rais Samia inayowajali wananchi wake na haitaki wapate kero hivyo imepunguza na kuwa mita 10 kwa kila upande.

Aidha amewataka wananchi wa maeneo ambayo barabara hiyo inapita, kutoa ushirikiano ikiwa ni kuunga Mkono juhudi za serikali kwa kuwa barabara hiyo inaleta maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

"Serikali imeshaleta fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii, haiwezekani ikacheleweshwa na watu wachache wasiotaka kubomoa nyumba zao, wananchi changamkieni fursa hiyo, kuna fursa pia ya ajira wakati ujenzi huu unavyoendelea " Amesema mkuu wa mkoa huyo.

Aidha, ameitaka Wakala wa barabara Tanzania (TANROAD) kuendelea kutoa elimu ya sheria ya barabara kwa wananchi ili waweze kuifahamu vizuri na kujenga uelewa wa pamoja.

Kwa upande wake, Meneja wa Wakala wa Barabara Mkoa wa Arusha Muhandisi Regnand Massawe amesema barabara hiyo ya Mianzini Sambasha ina urefu wa KM 12 na ile inayoanzia Olemringaringa hadi Ngaramtoni ina urefu wa KM 6 na kufanya jumla ya Km 18 na ujenzi unatarajiwa kukamilika ifikapo Agosti 2023.

Hata hivyo baadhi ya wananchi wameishukuru serikali kwa ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami na kuitaka serikali kusimamia sheria kwa usawa ili kukamilika kwa ujenzi wa barabara hiyo bila vikwazo.

"Serikali isimamie sheria kwa watu wote, wananchi tunataka maendeleo, hao wachache wanaokwamisha wachukuliwe hatua, ili wapishe ujenzi wa barabara uendelee, tumesubiri lami kwa muda mrefu, wakati umefika sasa". Amesema Zelote Aloyce mkazi wa Mianzini

Ziara ya kikazi ya Mkuu wa Mkoa ya kukagua ujenzi wa barabara ya Mianzini, Timbolo - Kinyaki hadi Ngaramtoni ilikuwa na lengo la kukagua ujenzi pamoja na kusikiliza changamoto za wananchi wa maeneo hayo.





# RAS ARUSHA AWASIHI WATUMISHI KUFANYA KAZI KWA USHIRIKIANO KAMA TIMU

**Na Elinipa Lupembe**

Katibu Tawala mkoa wa Arusha, Missaile Musa, amewataka watumishi kufanya kazi kwa weledi kwa kushirikiana pamoja kama timu, ili kufikia lengo la halmashauri na serikali kwa ujumla la kutoa huduma bora kwa wananchi.

Katibu Tawala huyo, ametoa rai hiyo wakati wa ziara yake ya kikazi katika halmashauri ya Arusha na kupata fursa ya kuzungumza na watumishi wa Makao Makuu, ikiwa na lengo la kukumbushana namna bora ya utekelezaji wa majukumu kwa watumishi wa Umma.

Katibu Tawala Missaile ameweka wazi kuwa licha ya kuridhishwa na kazi nzuri inayofanywa na watumishi wa halmashauri hiyo na kuufanya mkoa wa Arusha kuwa miongoni mwa mikoa inayofanya vizuri nchini, amewasisitiza kuendelea kuwajibika ipasavyo bila kukata tamaa.

Aidha amebainisha kuwa licha ya changamoto zinazojitokeza kukwamisha utekelezaji wa majukumu, amewahimiza kutumia rasilimali zilizopo na kuendelea kishirikiana kama timu moja, kuhakikisha wananchi wa mkoa wa Arusha wanapata huduma kupitia wao kama ilivyo lengo la serikali.

"Nafahamu kuna changamoto nyingi lakini zisitukwamishe wala kutukatisha tamaa, tuzigeuze kuwa fursa, niwasisitize kila mmoja kutimiza wajibu wake kwa kuzingatia kanuni, sheria na taratibu za utumishi wa Umma, tumieni taaluma zenu kwa kushirikiana kwa sekta zote kwa kuwa kila sekta zote inategemea sekta nyingine" Amesisitiza Maiselle

Hata hivyo watumishi halmashauri ya Arusha, wamepata fursa ya kuelezea changamoto zinazowakabili, katika kutimiza majukumu yao, na kumuamba katibu Tawala kushughulikia zile zilizo ndani ya uwezo wake jambo ambalo litaongeza ari ya wawatumishinkufanya kazi.

Naye Mkuu wa wilaya ya Arumeru, Mhandisi Richard Ruyango, amemshukuru katibu Tawala huyo na kuahidi kutekeleza maagizo yote ikiwa ni pamoja na kuwasimamia watumishi kutekeleza majukumu yao kwa weledi kwa kuzingatia taratibu za utumishi wa Umma.

"Watumishi hawa wanapambana sana kuhakikisha huduma kwa wananchi zinapatikana na zaidi tunamshukuru Rais wetu mama Samia Suluhu kwa kuboresha maslahi ya watumishi, ikiwemo kupandishwa kwa madaraja kwa watumishi wote ambao walikuwa wanastahili, nikuahidi hatutamuangusha mheshimiwa Rais". Amebainisha Mhandisi Ruyango

Awali katika ziara hiyo, licha ya kuzungumza na watumishi, katibu Tawala ametembelea miradi mimnee ya maendeleo katika sekta ya afya, elimu na miundombinu ya barabara.





# WANANCHI WA KIJIJI CHA BAWANI WASHIRIKI UJENZI WA NYUMBA YA MWALIMU SHULE SHIKIZI OLOKII

**Na Elinipa Lupembe**

Wananchi wa kijiji cha Bwawani kitongoji cha Olmapinuu, wakifanyakazi ya kuwasaidia mafundi kujenga nyumba ya mwalimu, kwenye shule shikizi Olokii, ujenzi unaotekelezwa na serikali kwa gharama ya shilingi milioni 50 fedha kutoka Serikali Kuu.

Wananchi hao, wamebainisha kufikia hatua hiyo, kutokana na kuona umuhimu wa nyumba hiyo ya mwalimu shuleni hapo, nyumba ambayo walimu wataishi hapo na kuwafundisha watoto wao kwa amani na utulivu.

Mjumbe wa kamati ya Mapokezi ya Ujenzi, Shaban Rashid amesema kuwa, watoto wao wamekuwa wakiteseka kwa miaka mingi, kutokana na shule ya msingi kuwa mbali na kutenganishwa na korongo ambalo wakati wa mvua watoto hushindwa kuvuka na kukosa masomo kwa zaidi ya miezi 4 mpaka 6 wakati mwingine.

"Tunamshukuru mama Samia, kweli amekikumbuka kijiji chetu hasa kitongoji cha Olmapinuu, kitongoji ambacho watoto wengi waliacha shule kwa kukata tamaa ya umbali na wengine kucheleweshwa kuandikishwa shule kutokana na wazazi kuhofia madhara watakayokutana nanyo njiani hasa kipindi cha mvua". Amefafanua Ally.

Aidha ameipongeza serikali kwa kuwashirikisha wananchi katika usimamizi wa miradi, jambo ambalo linawafanya wananchi, kumiliki miradi lakini linawafanya kujihakikishia matumizi sahihi ya pesa zao za Umma.

Awali Serikali inandelea na mkakati wa kuboresha miundo mbinu ya shule ili kuhakikisha watoto wenye umri wa kwenda shule, wanaandikishwa kwa wakati.





# MADIWANI WAIOMBA SERIKALI KUTUPIA MACHO UKARABATI NA UJENZI WA MIUNDOMBINU SHULE ZA MSINGI

**Na Elinipa Lupembe**

Baada ya Serikali kutoa fedha hivi karibuni kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari Nchini, waheshimiwa madiwani halmashauri ya Arusha wameiomba Serikali sasa kutupia macho katika upande wa shule za Msingi kwa kuanza utekelezaji wa ukarabati wa miundombinu chakavu hasa katika shule kongwe Pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa na vyoo katika baadhi ya shule hizo.

Hayo yamejiri wakati wa Kikao cha Waheshimiwa Madiwani cha kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli za maendeleo za Kata kwa robo ya kwanza ya mwaka wa Fedha 2022/2023 kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa halmashauri hiyo.

Wakiwasilisha taarifa za utekelezaji wa Kata, Waheshimiwa Madiwani wamewasilisha changamoto kubwa ya uchakavu wa miundombinu ya shuoe za msingi wamesema kuwa kuna uhitaji mkubwa wa ukarabati na ujenzi wa miundombinu katika shule za msingi, miundombinu ambayo ilijengwa miaka mingi iliyopita na kujenga hofu inayohatarisha usalama wa wanafunzi wenaosoma katika shule hizo.

Diwani wa kata ya Bangata Mhe. Ezra Tomito, amezitaja baadhi ya changamoto zinazokabili miundombinu ya shule za misngi ni pamoja na baadhi ya vyumba vya madarasa kuwa na sakafu ya udongo, uchakavu wa milango na madirisha, kuta na mapaa, uchakavu unaotokana na kujengwa na kutumika miaka mingi iliyopita hali inayopelekea wanafunzi katika shule hizo kuwa na wasiwasi kuhusu usalama wao.

"Baadhi ya shule zetu za Msingi zina ubovu wa miundombinu ambayo inahitaji ukarabati wa haraka kwa mfano, Shule ya Msingi Seliani yenye miaka zaidi ya mia moja (100) ni moja ya shule inayohitaji ukukarabati wa miundombinu yake karibu yote". Alisema Mhe. Eliakimu Marivey,

Diwani Kata ya Kimnyaki.Diwani wa kata ya Sokon II, Mhe. Obed Mollel, ameiomba na kuishauri Serikali kuanza kutenga fungu la fedha kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya shule za msingi kama inavyofanyika kwa shule za sekondari, ili wanafunzi waweze wapate masomo kwenye mazingira salama.

Akitolea ufafanuzi changamoto hiyo, Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Arusha Seleman Msumi, amesema kuwa Serikali imejipanga vizuri kwa ajili ya kutatua changamoto za miundombinu ya shule za msingi na hivi karibuni utakelezaji wa ukarabati wa miundombinu iliyochakaa pamoja na ujenzi wa vyumba vipya vya madarasa kwa shule zenye uhitaji utaanza ili wanafunzi wanaosoma katika shule hizo wasome kwa amani.

"Serikali inafahamu changamoto iliyopo katika miundombinu ya shule za Msingi hasa zile kongwe, na sasa kuna Mradi wa BOOST unaendelea kufanya tathmini ya uchakavu wa miundombinu kwa shule hizo, mara baada ya kukamilika kwake utatuzi wa changamoto hiyo katika shule za Msingi zenye uchakavu na uhaba wa vyumba vya madarasa utaanza kufanyiwa kazi". Alisema Mkurugenzi Msumi.

Sambamba na hayo, Mkurugenzi Msumi amesema kuwa serikali imejipanga kwa mwaka huu wa fedha kutekeleza miradi mbalimbali kisekta ikiwemo Sekta ya Afya katika hospitali ya Wilaya ya Oltrumet kwa kujenga Uzio pamoja na mahitaji mengine ya maabara, jingo la Mionzi pamoja jingo la Mochwari.

Awali Mkutano wa wazi wa Baraza la Madiwani umefanyika kwa mujibu wa sheria na kanuni za serikali za mitaa ukiwa na ajenda sita (6) huku ajenda kuu ikiwa ni kuwasilisha taarifa za utakelezaji wa shughuli za maendeleo za kata zilizofanyika kwa kipindi cha miezi mitatu.



# MAADHIMISHO YA SARATANI YA MATITI WANANCHI WAPATA ELIMU YA AFYA YA AKILI

Na Elinipa Lupembe

Wananchi husussani kina mama halmsahuri ya Arusha wamejitokeza kuadhimisha siku Saratani ya Matiti Duniani 2022 iliyofanyika kwenye hotel ya Olarndo Garden eneo la Sakina..

Kina mama hao licha ya kupata ufahamu na kupima bure Saratani ya Matiti na Mlango wa Kizazi, bure pamoja na magonjwa yasiyoambukiza, pia walipata fursa ya kupata elimu ya changamoto ya Afya ya Akili.

Katika dunia ya sasa watu wengi wanakabiliwa na changamoto ya afya ya akili bila kujifahamu na kujikuta wakipoteza mwelekeo wa maisha na kutengwa na ndugu, jamaa na marafiki.

Mratibu wa Afya ya Akili halmashauri ya Arusha, Dkt. Pascal Kang'ria, amefafanua kuwa changamoto ya afya ya akili matokeo ya sonona kali inayosababishwa msongo wa mawazo unaotokana na hali anazopitia mtu katika maisha yake ya kila siku.

Mara nyingi mtu mwenye changamoto ya Afya ya Akili huwa hajitambui kama ana tatizo, kwa kuwa wengi wao hujitenga na watu wao wa karibu na pengine kufanya vitu tofauti anavyohisi vinampa ahueni yeye bila kujali madhara yake kwa wengin

Kutokana na hali hiyo watu waliomzunguka kwa kutokujua tatizo lake, huanza kumshambulia na kumuona ana tabia zisizofaa, jambo ambalo humpoteza kabisa na wakati mwingine humsababisha hata kujiua.

Aidha Dkt. Kang'iria ameitaka jamii kufahamu dalili za changamoto ya Afya ya Akili kwa mtu binafsi na watu wao wa karibu ili kuweza kuzishughulikia kwa njia sahihi kwa bali kuzitatua kupitia tabia na mienendo ya mtu na jamii.

Amezitaja sababu za kawaida zinazomfanya mtu kupata changamoto ya akili ni pamoja na hali duni ya maisha, ukatili wa kingono utotoni, uonevu, ukosefu wa usawa kiuchumi na kijamii, unyanyapaa, ubaguzi na ukiukwaji wa haki za binadamu hususani kwenye maeneo ya kazi.

Aidha Dkt. Kang'iria ameweka wazi njia sahihi za kuepuka changamoto ya akili ni pamoja na kujikubali, kufahamu kuna kushinda na kushindwa, kuacha kuficha siri bali kuwa na mtu wa kumueleza siri zako, kutokukaa kimya, kuongeza marafiki, kupata muda wa kupumzika hasa kulala, na kufanya yale unayoyapenda, kujipa raha mwenyewe pamoja na kutoka na marafiki.

Inafahamika kuwa changamoto ya Afya ya Akili inaongezeka mwaka hadi mwaka, matokeo ya tafiti ya mwaka 2019, takribani watu bilioni 1 huku asilimia 14 ya vijana barurbaru duniani wanaishi na tatizo la akili, tatizo lilisababisha mtu 1 kati ya 100 kujiua na asilimia 58 ya watu wanaojiua ni watu wenye umri wa chini ya miaka 50.

Hata hivyo WHO inasema tatizo la akili ni sababu inayoongoza watu kupata ulemavu duniani, watu wenye tatizo la akili hufariki dunia miaka 10 hadi 20 mapema zaidi kuliko watu wa kawaida kutokana na magonjwa ya mwili yanayoweza kuzuilika.

Awali Halmashauri ya Arusha kwa kushirikiana na shirika la LUMINARY INC wamefanya Maadhimisho ya Wiki ya SARATANI YA MATITI Duniani 2022 yenye Kauli mbiu: "UTAMBUZI WA MAPEMA HUOKOA MAISHA", kwa kutoa huduma za upimaji bure kwa magonjwa yasiyoambukiza na yanayoambukiza ikiwemo Saratani ya Matiti na Saratani ya Shingo ya kizazi kwa siku tatu kuanzia tarehe 27-19 Oktoba 2022.




# WATOTO, WAZAZI KIJIJI CHA BWAWANI WAMSHUKURU MAMA SAMIA KUJENGA SHULE SHIKIZI OLOMAPINUU

**Na Elinipa Lupembe**

Wananchi hususani watoto na wazazi wa Kijiji cha Bwawani na vitongoji vyake, kata ya Bwawani halmashauri ya Arusha, wailaya ya Arumeru, wamemshukuru mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuwajengea madarasa kwenye shule shikizi ya Olokii katika kitongoji cha Olomapinuu.

Wananchi hao, wamefikia hatua hiyo mara baada ya serikali kutoa fedha kiasi cha shilingi milioni 90 kwa awamu mbili za ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na nyumba ya mwalimu, mishoni mwa mwaka 2021 ilitoa milioni 40 fedha za mapambano ya za UVIKO 19, zimejenga vyumba 2 vya madarasa na madawati 25 na mwaka 2022 ikitoa shilingi milioni 50 za ujenzi wa nyumba ya walimu.

Katika utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu hiyo, wananchi wa kijiji cha Bwawani wamejikuta wakisukumwa kuongeza nguvu kazi katika utekelezaji wa miradi hiyo ili iweze kukamilika kwa wakati na kuanza kutoa huduma kwa watoto na walimu wao.

Wakizungumza na mwandishi wetu, wananchi waliokuwa wakisaidia mafundi kujenga nyumba ya mwalimu, wamebainisha kuwa wamefikia hatua hiyo, kutokana na kuona umuhimu wa nyumba hiyo ya walimu, nyumba ambayo walimu wataishi hapo na kuwafundisha watoto wao.

Mjumbe wa kamati ya Mapokezi ya Ujenzi, Shaban Rashid amesema kuwa, watoto wao wamekuwa wakiteseka kwa miaka mingi, kutokana na shule ya msingi kuwa mbali na kutenganishwa na korongo ambalo wakati wa mvua watoto hushindwa kuvuka na kukosa masomo kwa zaidi ya miezi 4 mpaka 6 wakati mwingine.

"Tunamshukuru mama Samia, kweli amekikumbuka kijiji chetu hasa kitongoji cha Olmapinuu, kitongoji ambacho watoto wengi waliacha shule kwa kukata tamaa ya umbali na wengine kucheleweshwa kuandikishwa shule kutokana na wazazi kuhofia madhara watakayokutana nanyo njiani hasa kipindi cha mvua". Amefafanua Ally.

Aidha ameipongeza serikali kwa kuwashirikisha wananchi katika usimamizi wa miradi, jambo ambalo linawafanya wananchi, kumiliki miradi lakini linawafanya kujihakikishia matumizi sahihi ya pesa zao za Umma.

Hata hivyo wanafunzi wa shule hiyo shikizi, wameipongeza na kuishukuru serikali na kudai kuwa kwa sasa wanasoma kwenye madarasa mazuri, na watoto wengi wanapata fursa ya kuanza shule kwa wakati.

Yunus Alley mwanafunzi wa darasa la awali, amesema kuwa kwa sasa wanasoma kwa furaha, madarasa ni mazuri, shulemiko karibu na nyumbani.

Akitoa ushuhuda wa kuanza kwa shule hiyo mwalimu Zakayo Lukumai, ameema shule ilianza mwka 200 kwa wanafunzi kukaa chini,na baadaye kupata darasa la nyasi, mwaka 2022 serikali imejenga madarasa mawili mazuri, madarsa ambayo yamesababisha ongezekomla wanafunzi shule hapo.

"Kwa sasa tuna ongezeko la wanafunzi, wamefikia 110, kutoka wanafunzi 40 hapo awali, kwa sasa wazazi wamepata mwamko wa kuwaandikisha watoto kuanza shule". Amesisitiza Mw. Lukumai

Awali Serikali inandelea na mkakati wa kuboresha miundo mbinu ya shule ili kuhakikisha watoto wenye umri wa kwenda shule, wanaandikishwa kwa wakati.



# MKAKATI WA KUTHIBITI MINYOO YA TUMBO KWA WATOTO WA MIAKA 5- 14

**Na Elinipa Lupembe**

Halmashauri ya Arusha, imeanza mkakati wa kutekeleza mpango jumuishi wa Taifa wa kudhibiti Magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, kwa watoto wenye umri wa kuanzia miaka 5 mpaka 14, walioandikishwa shule na wasio kwenye mfumo wa shule.

Akizungumza wakati wa kikao kazi hicho, Katibu Tawala wilaya ya Arumeru, Mwl. James Mchembe, ameitaka timu ya watalamu iliyoteuliwa kuhakikisha wanafanya kazi hiyo kwa bidii na kwa kushirikiana ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

"Huu ni mpango wa kitaifa, tunatakiwa kuhakikisha tunatekeleza shughuli hii kila mmoja kwa nafasi yake, ili kufikia malengo ya serikali ya kuwakinga watoto ambao wako kwenye hatari kubwa ya kuambukizwa magonjwa ya minyoo tumbo ili kuwaandaa watoto kuwa na Taifa lenye watu wenye afya bora hapo baadaye". Amesisitiza Katibu Tawala huyo.

Aidha Katibu Tawala huyo, amewataka watalamu licha ya kutoa dawa kinga hizo, ni vema kujikita pia kutoa elimu ya usafi kwa jamii, ili kujikinga na minyoo kwa kuwa na vyoo bora pamoja na kuwa na tabia chanya za afya za kunawa mikono kwa maji safi na sabuni kabla ya kula, kabla ya kunyonyesha mtoto, wakati wa kumtawaza mtoto na mara baada ya kutoka chooni pamoja na watoto kuvalishwa viatu.

Hata hivyo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha, mhe. Ojung'u Salekwa, ameishukuru serikali kwa mpango huo mpango ambao una manufaa makubwa kwa watoto, wananchi na jamii kwa ujumla wake.

"Ninaipongeza serikali, ninamshukuru mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa na mpango wa kuandaa watoto wenye afya bora, watoto ambao ni wajenzi wa Taifa la kesho, mtoto asiyeshambuliwa na magonjwa afya yake ya akili inayomuwezesha mtoto kulitumikia taifa lake akiwa na afya bora" Amesisitiza Mwenyekiti Ojung'u

Mganga mkuu halmashauri ya Arusha, Dkt. Peter Mboya, ameweka wazi kuwa, halmashauri inategemea kutoa kinga tiba ya minyoo tumbo kwa watoto 80,000 wa kuanzia miaka 5 mpaka 14, walio kwenye mfumo wa shuleni na wasio kwenye mfumo wa shule.

Amefafanua kuwa makusudi ya mpango ni kuendeleza mpango jumuishi wa Taifa wa kudhibiti magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele ukiwa na dira ya kuwa na jamii yenye afya bora na ustawi na usiyodhoofisha na madhara ya magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele.

Mratibu wa magonjwa yasiyo ya kuambukizwa halmashauri ya Arusha, Ramadhani Kulewa, amesema kuwa halmashauri inategemea kutoa kinga tiba ya ugonjwa wa minyoo tumbo kupitia vituo 211, vituo vya afya 56 na kwenye shule za msingi 155 huku wahudumu 433 wakiwemi walimu 310 na wahudumu wa afya 112.

Kulewa aethibitisha kuwa ili kufikia lengo, licha ya kuwa na vituo hivyo maalum halmashauri pia itatumia mfumo wa ugawaji dawa katika jamii kwa kupita nyumba kwa nyumba, ugawaji wa dawa kwa makundi maalum, pamoja na kwenye mikusanyiko ya watu kama nyumba za ibada, sokoni, vituo vya mabasi na meeneo yote ya biashara.

Awali halmashauri ya Arusha inategemea kuwapatia kinga tiba ya minyoo kwa watoto 80,000, watoto 76,000 kati yao ni wale waliosajiliwa shuleni na watoto 4,000 ni ambao hawajasajiliwa kwenye mfumo rasmi wa elimu.



# WADAU WA ELIMU WAJADILI MKAKATI WA KUENDELEZA SEKTA YA ELIMU

**Na Elinipa Lupembe**

ASAS za kiraia zinazojihusisha na masuala ya elimu, halmashauri ya Arusha, wamekutana na kujadili mstakabali wa elimu na kupanga mkakati wa pamoja namna bora ya kuboresha na kuendeleza sekta ya elimu bila kuathiri sheria na sera ya elimu nchini.

Wadau hao, wamekutana katika kikao kazi cha siku moja kilichofanyika kwenye ukumbi wa shule ya msingi Green Acres, kikiwa na lengo la kubadilishana uzoefu kati ya idara za elimu za halmashauri na ASAS za Kiraia ili kuwa na uelewa wa pamoja na kuanda mkakati wa kuendeleza sekta ya elimu.

Akizungumza wakati wa kufungua kikao kazi hicho, Katibu Tawala wilaya ya Arumeru, Mwl. James Mchembe, amebainisha kuwa serikali imetoa fursa kwa ASAS za kiraia kushiriki katika kutekeleza mpango mkakati katika sekta ya elimu, hii ni kutokana na ukubwa wa mahitaji usioendana na uwezo wa kirasilimali.

Amesema kuwa ASAS za kiraia ni kiungo cha msingi sana katika kutekeleza vipaumbele vya serikali vya kutoa huduma za jamii kisekta na kusisitiza kuwa, licha ya kuwa serikali inatekeleza majukumu yake lakini mafanikio ya elimu nchini yanapewa nguvu na ASAS za kiraia.

"Serikali inathamini kazi zenu mnazozifanya kwa niaba ya serikali, natumaini matokeo ya kikao kazi hiki, yanaenda kutoa suluhishi na dira ya utatuzi wa changamoto za elimu, kwa lengo la kumkomboa mtoto kifkra kupitia elimu".Amefafanua Mwl. Mchembe.

Maafisa Elimu Msingi na Sekondari, walielezea dira, maono, malengo na mwelekeo wa elimu katika halmashari hiyo na kubainisha changamoto zinazokwamisha kufikia malengo ikiwemo upungufu wa miundombinu, utoro unaosababishwa na ukosefu wa chakula kwa shule za kutwa, watoto kuchelewa kuandikishwa shule kutokana na umbali wa shule pamoja na uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa elimu ya awali.

Hata hivyo wadau hao, wameupongeza uongozi wa halmashauri hiyo kwa kuona umuhimu wa kukaa pamoja na kupanga mipango ya pamoja yenye kunia mamoja katika kutekeleza mikakafti ya elimu na kufikia malengo ya serikali.

Hata hivyo, wadau hao wa elimu, wameahidi kushirikiana na halmashauri, kuhamasisha wazazi na jamii kutambua majukumu yao kwa watoto wao ikiwemo suala la kuchangia vhakula cha watoto wanaosoma shule za kutwa.

Mratibu wa miradi, shirika la ACE Africa, Bugesi Matayo amebainisha kuwa, wazazi wamekuwa na mawazo potofu juu ya sera ya elimu bure, na kujiweka pembani na kuacha kuwahudumia watoto wao husuani kuwahudumia chakula cha mchana kwa wanafunzi wa kutwa.

Aidha Wadau hao wa Elimu wamekubaliana kwa kukaa pamoja na uongozi wa Halmashauri ya Arusha, kupanga mipango ya pamoja kwa mwkaa ujao wa masomo unaoanza 2023, ikiwa na lengo la kuboresha sekta ya elimu kwa kutatua changamoto zanazowakabili wanafunzi shuleni.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji, halmashauri ya Arusha Selemani Msumi amezisisitiza ASAS za Kiraia kutokuchoka kuisaidia jamii hususani watoto ambao wanaoandaliwa kulitumikia taifa hili huku wakiwa na ndoto za kutimiza katika maisha yao kupitia elimu,zaidi ni utekeleazaji wa ilani ya CCM wa kuimarisha mashirika ya Umma ili yaweze kuendelea kutoa, michango katika maendeleo ya Taifa.

"Tunafahamu elimu ni msingi wa maisha, Wadau mnalo jukumu la kushirikiana na serikali kuhakikisha watoto wanapata elimu bora, katika mazingira bora bila vizuizi vinavyoweza kuzilika, tukiunga kwa pamoja, tukania mamoja katika kusukuma gurudumu hili la elimu kwa mtoto wa kitanzania, tutafikia malengo ya serikali ya kuoambana na adui ujinga, umasikini na maradhi". Amesisitiza Msumi



# VIJANA 92 WAHITIMU MAFUNZO YA JESHI LA AKIBA ARUMERU

**Na Elinipa Lupembe**

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Mhandisi Richard Ruyango leo ameitimisha Mafunzo ya Jeshi la Akiba (Mgambo) kwenye hafla iliyofanyika Kata ya Bwawani Halmashauri ya Arusha.

Katika hafla hiyo jumla ya vijana 92 kata ya vijana 147 waliandikishwa kuanza mafunzo hayo tarehe mapema mwezi Agosti, 2022 huku wanawake wakiwa 10 na wanaume 82.

Akizungumza wakati wa kufunga mafunzo hayo, Mkuu wa wilaya ya Arumeru amewaasa vijana wote waliomaliza mafunzo hayo, kuwa watii na wazalendo kwa Taifa lao na kuhakikisha wanatumia maarifa waliyoyapata kuendeleza amani na utulivu katika nchi hii.

Aidha amewakumbusha utii kwa viongozi wote na kwa kuwa Mhe.Rais Rais wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka mfumo mzuri wa majeshi ya Ulinzi na wao kwa sasa ni sehemu ya Ulinzi wa Taifa.

"Tumieni mafunzo haya kulitumika Taifa na zaidi katika kulinda raia na mali zao na siyo kuvunja sheria za nchi, kwa serikali imewaamini na kuwapa mbinu za ulinzi na usalama wa raia, hiyo jukumu lenu kubwa ni kuwatumikia wananchi". Amesema Mkuu huyo wa Wilaya

Mkufunzi wa Mgambo Wilaya ya Arumeru Meja Khamis licha ya kumshukuru Mkuu wa Wilaya kwa kukubali kuja kufunga Mafunzo hayo amewapongeza wakufunzi wote waliofanikisha Mafunzo ikiwa ni pamoja na kuitaka jamii kuwapa vijana hao ushirikiano pindi watakaporudi katika maeneo yao.

Ameongeza kuwa, vijana hao 92 pamoja na mafunzo ya Kijeshi waliopata, walipata pia mafunzo kutoka Jeshi la Uokoaji na Zima Moto, Takukuru, Mafunzo ya Kareti, Mafunzo ya Jeshi la Uhamiaji na Mafunzo ya Kupambana na Dawa za Kulevya, mafunzo ambayo yamewapa mbinu na maarifa ya ulinzi wa raia na mali zao.



Wakisoma Risala yao kwa mgeni sasmi, vijana hao wameiomba serikali kuupa fursa ya mafunzo hayo mara kwa mara ili kukuza na kuendeleza maarifa na ujuzi katika kazi.

Aidha wakaiomba serikali kuwaunganisha na mashirika na makampuni ya ulinzi ili waweze kupata ajira pamoja na kuwapa kipaumbele kwenye kazi maalumi za serikali kama vile uchaguzi, wakati wa mitihani.

Hata hivyo, Taasisi za Ulinzi zikiongozwa na SUMA JKT Sajenti Ndege, amemuahidi mkuu wa wilaya kuwachukua vijana 50 ili kuwapatia ajira kwenye kampuni ya SUMA JKT inayomilikiwa na Jeshi la Kujenga Taifa.

Katika sherehe hizo mkuu wa wilaya aliambatana nawajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, viongozi wa halmashauri za Arusha na Meru, viongozi wa Chama, viongozi wa dini na wa siasa pamoja na wananchi wa halmashauri zote mbili.



# SIKU 16 ZA KUPINGA UKATILI WA KIJINSIA WATOTO WA KIUME WAFANYA TATHMINI

**Na Elinipa Lupembe**

Katika kilele cha Siku 16 za kupinga ukatili wa Kijinsia, halmashauri ya Arusha, imefanya kikao kazi cha tathmini ya matukio ya ukatili wa kijinsia huku takwimu zikionyesha watoto wakiume wakiwa kwenye hatari kubwa ya kufanyiwa ulawiti.

Katika kikao hicho watoto walipata fursa ya kuelezea namna Klabu zao zinavyowawezesha kujitambua na jinsi ya kujikinga na kukaniliana na matukio ya ukatili hususani ulawiti kwa watoto wa kiume pamoja na changamoto wanazokabiliana nazo katika kuelemishana wao kwa wao.



Watoto hao wamesema kuwa kupitia klabu hizo, wamejengewa uwezo na wameweza kutumia maarifa hayo kuelemisha wenzao shule na nyumbani pia, mafanikio ambayo yameanza kuwafanya watoto wa kiume kuanza kutambua hali halisi ya ulawiti unaoendelea kwenye jamii.

Hata hivyo wamebainisha baadhi ya changamoto zinazowakabili watoto ni pamoja na wazazi kukosa muda wa kukaa na watoto wao, mila na desturi pamoja familia kuwaamini ndugu, jamaa na marafiki, watu ambao ndio wanaowafanyia watoto ukatili huo.

Awali katika kikao kazi hicho, kimefanikiwa kuweka malengo ya utekelezaji wa kupambana na matukio ya kingono dhidi ya watoto na kukubaliana kuwalinda watoto wate na sio watoto wa kike peke yao.



Kikao kazi hicho kilichowakutanisha viongozi wa klabu za watoto wa kiume 'Boys Vac Lab' shule sita za msingi, walimu walezi wa klabu hizo, wanasheria, mawakili, Polisi Dawati la jinsi pamoja na watalamu wa Halmashauri hiyo.

Halmashauri kwa kushirikiana na shirika la CWCD inatekeleza mradi wa kwanza wa kupinga ukatili wa kingono kwa watoto wa kiume, kupitia klabu za 'Boys Vac Lab' kwenye shule sita za msingi kwa ufadhili wa Foundation for Civil Society.





# RUZUKU YA TASAF YAWEZESHA KAYA KUPATA MITAJI YA BIASHARA

**Na Elinipa Lupembe**

Fedha za ruzuku zinazotolewa na serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF na mpango wa Kunusuru Kaya Masikini, zimeanza kuzaa matunda kwa kuwawezesha wanufaika wa mpango huo, kuanzisha biashara ndogo ndogo na kujikimu na hali ngumu ya maisha.

Wanufaika hao, wamekutwa na mwandishi wetu, wakiwa kwenye biashara ya nguo za mitumba, wakati wa kupokea ruzuku ya fedha za ruzuku kwa mwezi wa 7/8 mwaka 2022, kwenye ofisi ya Kijiji cha Laroi kata ya Laroi, halmashauri ya Arusha, wilaya ya Arumeru.

Aidha wanufaika hao wameelezea hisia zao kwa serikali kupitia TASAF, namna imezitoa kaya hizo kwenye hali ngumu ya kiuchumi ya kushindwa kumudu hata kupata mahitaji ya lazima kwa familia zao, na kuongeza kuwa kwa sasa wameanza kusahau mateso hayo.

"Tunamshukuru Mungu, tunamshukuru Mama Samia, ameleta neema kwa kina mama, amekuwa ni mfano kwa kina mama, kila mama anajiamini kupitia Mama Samia, kama Rais anafanya kazi kwa nini sisi tusifanye, hakuna mwanamke analala siku hizi, TASAF imetutoa gizani". Wameweka wazi kina mama hao

Zaina Ebeneza (32) mnufaika wa TASAF kijiji cha Laroi na mama wa watoto watano, amebainisha kuwa amekuwa akopokea ruzuku ya shilingi 54,000, fedha iliyomuinua kutoka kwenye lindi la umaskini uliokithiti na kumuwezesha kupata mtaji wa kuuza nguo za mitumba.

"Ninauza nguo kwa kutembeza lakini pia ninauza kwenye minada siku ya soko, TASAF imenitoa mbali sana, nilikuwa na hali ngumu sana kimaisha, nina watoto watano wananitegemea, kwa sasa hali yangu imeimarika, ninafanya biashara yangu na ninapata mahitaji ya familia, watoto wanasoma na kupata mahitaji yao kama watoto wengine". Amesema Zaina

Naye Ester Lobulu ( 50) mfanyabiashara wa nguo na mbogamboga, amesema kuwa analea watoto na wajukuu watatu, mmoja ni yatima, ruzuku ya TASAF imemsaidia kufanya biashara nguo, siku za soko la Mirongo, nasiku za kawaida huuza mboga kwa kutembeza majumbani.

"Tunamshukuru Mungu, tunamshukuru mama Samia, TASAF imetusaidia hasa wamama, tulikuwa tunateseka na maelezi ya familia, mume aliniacha na akaniachia watoto, ninawasomesha, maisha sio magumu sana kwa sasa ninapambana na Mungu ananisaidia, siku za mnada nauza nguo Mirongoine, siku za kawaida natembeza mboga kwenye nyumba za watu". Amesema Ester.

Ifahamike kuwa Mpango wa kunusuru kaya masikini unalenga kuziwezesha kaya kuondokana na umasikini uliokithiri kwa kupambana na adui ujinga, umasikini na maradhi kupitia ruzuku ya msingi ya kuiwezesha kaya kupata mahitaji ya chakula na mavazi, ruzuku ya elimu ya kuhakikisha watoto wa kaya wa kuanzia miaka 7- 18 wanapata elimu ya msingi huku watoto wa miaka 0-5 wanapata huduma za afya kwa kuhudhuria kliniki nankupata chanjo kwa kipindi chote.





# WILFRED DANIEL AWA MWENYEKITI MWENZA WA BARAZA LA BIASHARA WILAYA YA ARUMERU

**Na Elinipa Lupembe**

Mfanyabiashara Wilfred Daniel amechakuguliwa kuwa Mwenyekiti Mwenza wa Baraza la Wafanya biashara wilaya ya Arumeru baada ya kushinda kwenye uchaguzi uliofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa halmasahuri ya Meru, Baraza linalojumuisha halmashauri za Arusha na Meru zinazounda wilaya ya Arumeru.

Mfanya biashara huyo amepata nafasi hiyo, na kupewa dhamana ya kuliongoza Baraza hilo kwa kipindi cha miaka 3, kwa kupata kura 19 kati ya kura 49 zilizopigwa na kuwashinda wagombea wenzake watatu waliowania nafasi hiyo.

Awali Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyabiashara wilaya ya Arumeru ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Mhandisi Richard Ruyango, kwa mujibu wa Kanuni, amemtangaza Mfanyabiashara Wilfred Daniel kuwa Mwenyekiti mwenza wa Baraza hilo, huku akimtangaza Makamu Mwenyekiti Mwenza CPA. Maija Mchau aliyepata kura 17.

Aidha Mhandisi Ruyango, amewataka viongozi hao kusimamia miongozo na kuyafahamu madhumuni ya Baraza ili kuweka mkakati wa utekelezaji na kuyafikia malengo ya baraza kwa kushirikishana kutatua changamoto zinazowakabili wafanyabiashara kwa maendeleo ya wananchi na Taifa.

"Serikali inatambua huduma mnayoitoa kwa jamii, ninawaagiza viongozi, kaeni na wafanyabiashara wenzenu mpate maoni yao, ili kuishauri serikali namna bora ya kuenenda ili kuwa na mazingira rafiki ya kuendesha biashara, yanayochochea maendeleo binafsi na ya Taifa". Amesisitiza mkuu huyo wa wilaya

Hata hivyo baada ya uchaguzi huo, Mwenyekiti mwenza licha ya kuwashukuru wajumbe kwa kumuamini na kumpa nafasi hiyo , ameahidi kushirikiana na wafanyabiashara wote kwa kuitumikia nafasi hiyo kwa uaminifu ili kufikia lengo la serikali kupitia Baraza la wafanayabishara la kuwaunganisha na serikali.

Mkuu wa Idara ya Biashara na Uwekezaji, halmashauri ya Meru, Noel Pallangyo ameyataja madhumuni ya Baraza la Biashara la wilaya ni kuwakutanisha Sekta Binafsi na Serikali ili kujadili na kupeana ushauri wa namna ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji katika Wilaya na kukuza sekata ya uchumi.

Majukumu mengine ni pamoja na kutengeneza mazingira bora ya kufanyia Biashara na uwekezaji, Kuibua fursa za uwekezaji, kuzinadi fursa hizo kupitia makongano mbalimbali pamoja na kufanya matangazo ya biashara.

Baraza la Taifa la Biashara la wilaya lilianzishwa chini mwaka 2001 kwa waraka wa Rais na 1 wa mwaka 2001 ukielekeza kila wilaya liunde Baraza la Biashara la Wilaya ikiwa ni jitihada ya kukuza uchumi ndaninya wilaya, wilaya ya Arumeru imeunda Baraza hilo na kuchagua viongozi watakaoongoza kwa miaka miatatu.







# KINAMAMA WAMSHUKURU MAMA SAMIA KWA MIONGOZO YA ELIMU

**Na Elinipa Lupembe**

Wananchi wa kata ya Laroi halmashauri ya Arusha, wamefanya uzinduzi wa Miongozo ya Elimu iliyotolewa na serikali, huku kina mama wa kata ya hiyo, wakiipongeza serikali ya awamu ya sita na kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzani Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa miongozo ya elimu itakayomuwezesha mtoto wa kike kwenda shule.

Kina mama hao wametoa pongezi kwa kuwa miongozo hiyo, imeweka wazi ushiriki wa wazazinkatikamkutekelza sera ya elimu pamoja na ulazima wa kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule aandikishwe na kuhakikisha amemaliza elimu ya msingi ya kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha nne.

Wamesema kuwa, watoto wao watapata fursa ya kuendelea na masomo fursa ambayo kina mama hao wanakiri kutokuipata kutokana na mila na desturi za kabila lao la kimaasai, ambapo watoto wa kike walikuwa wakiishia darasa la saba na kuolewa.

Serikali imetoa mwongozo ambao utawabana wazazi kuwapeleka watoto wote shule, miongozo ambayoo utatoa haki hususani kwa watoto wa kike ambao waliikosa fursa hiyo miaka iliyopita na kuweka wazi kuwa kina mama watahamasishana kuhakikisha watoto wao wanasoma shule kama ilivyokuwa kwa watoto wa kiume.

Hosiana John (mama Lucas Julias) amebainisha kuwa, yeye hakupata nafasi ya kusoma, lakini hujisikia fahari sana anapoona mwanamke msomi, zaidi amepata hamasa zaidi kuwa na Rais mwanamke, na kuahidi kupambana kuhakikisha watoto wake wa kike wanasoma katika jamii yao.

"Kina mama tusirudi nyuma, tupambane kufanya kazi watoto wetu wasome, tulime, tuuze nyanya, vitunguu ili mrafi tuwawezeshe watoto wetu wasome, kama wengine, maendeleo ya kijiji chetu yanaletwa na wasomi hivyo wasomi hao wawe ni watoto wetu". Amesisitiza Mama Hosiana.

"Miongozo hii ingekuja kipindi chetu, hata mimi ningesoma, nimeishia darasa la saba na sikuwa mjinga, nilikuwa nashika nafasi nzuri darasani ila sikupata fursa kama hii, nitahakikisha watoto wangu wanasoma bila kubughudhiwa na kufikia ndoto zao, ninatamani kuona familia zenye vijana wasomi, tutashiriki kuhakikisha watoto wetu wanasoma". Ameweka wazi Dorah Dorian.

Naye Afisa Mtendaji wa Kata ya Laroi, Mneji Bugwema amebainisha kuwa, wananchi wa kata ya Laroi wamepokea miongozo hiyo na kuahidi kushiriki katika utekelezaji wake, hususani kwenye eneo la ushiriki wa wananchi katika kuboresha sekta ya elimu sambamba na kuinua kiwango cha taaluma kwa wanafunzi na kufikianlengonla serikali.

"Miongozo ya elimu imeweka wazi taratibu zote za elimu na malengo yake pamoja na majukumu ya kila mdau wa elimu, kuanzia wanafunzi, walimu, wazazi paomja na viongozi wasimamizi wa elimu, kwa kushirikiana kutekeleza miongozo hiyo kilammmoja kwa nafasi yake, tutafikia malengo ya serikali ya kukuza sekta ya elimu nchini".Amefafanua Afisa Mtendaji huyo

Ikumbukwe kuwa serikali imetoa miongozo mitatu ya elimu itawapa fursa wazazi na walimu kushiriki katika malezi na maadili ya watoto, usimamizi wa wazazi kuchangia chakula cha watoto shuleni, ujenzi na utunzaji wa miundombinu ya shule pamoja na namna bora ya uteuzi wa viongozi wasimamizi wa elimu.



# SERIKALI YAIMARISHA MIUNDOMBINU YA SHULE CHANGA SEKONDARI LOSINONI

**Na Elinipa Lupembe**

Licha ya kuwa Serikali inaendelea na mkakati wa kukarabati shule kongwe za sekondari bado imejikita katika kuziimarisha shule changa kwa kuongeza miundo mbinu ili zikamilike, lengo likiwa ni kuhakikisha watoto wote nchini, wanapata elimu ya sekondari katika maene yao.

Shule ya sekondar Losinoni ni miongoni mwa shule changa za kata iliyoanza mwaka 2020 kwa kuusajiliwa kwa namba S. 5347, ikiwa umbali wa takribani Kilomita 45 kutoka makao makuu ya halmashauri ya Arusha.

Akizungumza na mwandishi wetu, Mkuu wa shule ya sekondari Losinoni Mwl. Emanuel Mkonongo, amethibitidha kuwa serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule hiyo huku mwaka huu wa fedha ikiwa imepokea shilingi Milioni 40 kutoka serikali kuu za ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa, viti na meza 80 na kufanikiwa kujenga na ofisi ya walimu kwenye jengo hilo na ujenzi ukiwa umekamiliaka.

Imeelezwa kuwa, shule hiyo ilianzishwa kwa nguvu za wananchi na ufadhili wa Hifadhi ya Wanyamapori Arusha (ANAPA) kutokana na asilimia kubwa ya watoto wa eneo hilo hususani wasichana kushindwa kuendelea na elimu ya sekondari kutokana na umbali mrefu ilipokuwa shule ya sekondari.

Kutokana na juhudi na ari ya wananchi wa Losinoni, serikali ilianza kuwekeza nguvu na kuongeza kasi ya ujenzi wa miundo mbinu ya shule hiyo pamoja na usajili wa shule hatimaye Januari 2020, wanafunzi walipangiwa shuleni hapo kuanza kidato cha kwanza.

Mkonongo ameongeza kuwa, Serikali imeendelea kuwekeza miundombinu ya shule hiyo na kuifanya iendelee kukua kwa manufaa ya watoto wa kijiji cha Losinoni, mpaka sasa shule ina wanafunzi 202 wa kidato cha kwanza mpaka cha tatu ikiwa na vyumba 10 vya madarasa, matundu ya vyoo, maabara za masomo ya Kemia na Baiolojia, na Fizikia na Jiografia, pamoja na nyumba 2 za walimu za (2 in 1).

"Licha ya kuwa shule hiyo ni changa lakini juhudi kubwa za serikali zinaifanya shule hiyo kuwa bora kwa upande wa miundo mbinu, huku wadau wengine wa maendeleo wakiendelea kutoa vifaa vya kujifunzia na kufundishia ikiwemo wanafunzi wasomi wenyeji wa kijijini hapo" Amesisistiza Mkonongo

Awali Serikali imetoa shilingi milioni 760 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 38 kwa 15 za sekondari halmashauri ya Arusha, ikiwa ni maandalizi ya kuwapokea wanafunzi wa kidato cha kwanza Januari 2023.

Ifahamike kuwa, mradi huu ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi Ibara ya 79 kifungi (i) ikijibainisha kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya sekondari kwa kuongeza idadi ya shule za sekondari, kuboeresha mazingira ya kujifunzia wanafunzi lengo likiwa kuongeza ufaulu wa wananfunzi wa kidato cha nne.





# VIONGOZI WAMSHUKURU MAMA SAMIA MGAO WA PIKIPIKI ZA LISHE

**Na Elinipa Lupembe**

Uongozi wa halmashauri ya Arusha, umemshukuru mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan na Serikali ya awamu ya sita kwa kutoa pikipiki kwa ajili ya ufuatiliaji wa masuala ya Lishe hususani watoto wenye utapiamlo.

Akizunguza wakati wa kukabidhi pikipiki hizo kwa watalamu wa Idara ya Afya, Mkurugenzi Mtendaji halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, amemshukuru mheshimiwa Rais kwa mgao huo wa pikipiki, vitendea kazi ambavyo vitarahisisha ufuatiliaji wa watoto wanaokabiliwa na changamoto ya utapiamlo.

"Tunamshukuru Mama Samia, tumegawa pikipiki hizi kwenye maeneo ambayo yana idadi kubwa ya watoto wenye utapiamlo, licha ya kwamba zitawasaidia watalamu wetu lakini zitarahisisha upatikanaji wa huduma kwa wepesi kwa watoto wenye utapiamlo". Amesisitiza Mkurugenzi huyo.

Afisa Lishe halmashauri ya Arusha, Doto Milembe, amethibitisha kuwa, mgao wa pikipii hizo umezingatia maeneo yenye idadi kubwa ya watoto wenye utapiamlo mkali kwa lengo la kuwarahisishia watalamu kufanya ufuatiliaji kwa watoto waliopatiwa matibabu kwa kushirikiana na wahudumu ngazi ya jamii.

"Pikipiki hizo zitakuwa msaada mkubwa kwa watalmu kuweza kuwafikia watoto kwenye kaya, kufanya ukaguzi wa vyakula pamoja na upimaji wa madini joto kwenye chumvi shuleni na madukani, pamoja na kufanya kufanya tathmini ya kwenye kaya". Amefafanua Doto

Hata hivyo watalamu waliokabidhiwa pikipiki hizo, wameishukuru serikali ya awamu ya tano, inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan kwa kutoa vitendea kazi hivyo, vitakavyorahisisha utekelezaji wa majukumu yao kwa jamii.

Nuru Ally, Muuguzi wa zahanati ya Nameloki, kijiji cha Losinoni Juu, ameweka wazi kuwa, licha ya pikipiki hiyo kumrahisishia usafiri wa kuwafikia watoto, itaongeza tija na ufanisi katika kazi ya kuwahudumia watoto wenye utapiamlo pamoja na kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa lishe bora kwa watoto.



"Hiki ni kitendea kazi cha muhimu kutokana na changamoto ya ugumu wa kufikika kwa baadhi ya maeneo katika kata ya Musa, pikipiki itaniwezesha kuwafika na kuwahudumia watoto wengi kwa muda mfupi, tofauti na hapo awali". Amesisitiza Lugito Nzala Muuguzi Zahanati ya Musa

Ifahamike kuwa serikali imetoa pikipiki kwa halmashauri zote nchini kwa ajili ya ufuatiliaji wa masuala ya Lishe, hususani kwa watoto wenye utapiamlo mkali, huku halmashauri ya Arusha ikiwa ni miongozi mwao kwa kuoata jumla ya pikipiki tatu.





# PSSSF YATETA NA WATUMISHI KUHUSU KIKOKOTOO

**Na Elinipa Lupembe**

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), wamekutana na watumishi wa Makao Makuu, halmashauri ya Arusha, kwa lengo la kukumbushana majukumu na wajibu wa mfuko kwa watumishi pamoja na mabadiliko ya mfuko, ikiwemo kikokotoo cha mafao ya kustaafu.

Akizungumza kwenye kikao kazi hicho kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa halmashauri hiyo, Afisa Mwandamizi PSSSF Kanda ya Kaskazini, Venance Mwaijibe, amesema kuwa, Mfuko wa PSSSF una jukumu la kuwahudumia watumishi wa Umma hivyo watumishi wanapaswa kuufahamu mfuko na huduma wanazostahili kupata wakiwa kwenye ajira na sio mpaka kustafu.

Mwaijibe ambainisha kuwa watumishi wengi hufika ofisi za PSSSF pindi wanapolazimika kuanza kufuatilia mafao ya kustaafu, jambo ambalo si sahihi, mtumishi anatakiwa kufika na kuufahamu mfuko mara anapoanza makato na kuendelea kufuatilia mpaka pale anapofikia muda wa kustaafu.

Aidha ameyataja mafao yanayotolewa na mfuko ni pamoja na uzee, uzazi, ugonjwa, ulemavu, kukosa ajira na warithi, na kufafanua kuwa baadhi ya mafao si lazima mtumishi awe amestaafu utumishi wa Umma.

Aidha ametoa ufafanuzi wa maana halisi ya kikokotoo cha asilimia 33 na kufafanua kuwa, kuanzia tarehe 01 Julai, 2022, mtumishi atakapostaafu atapatiwa fao la mkupuo la asilimia 33 na kuendela kupata fedha kwa mwezi kipindi chote cha maisha yake kwa kuzingatia kanuni za kikokotoo cha hesabu za mfuko.

Hata hivyo Mkurugenzi Mtendaji, amelishukuru shirika hilo kwa elimu waliyoitoa kwa watumishi, elimu ambayo imefungua wigo na uelewa mpana wa kufahamu wajibu wa mwajiri na haki za mtumishi, elimu ambayo inapaswa kutolewa mara kwa mara kwa watumishi ili kuondoa sintofahamu kwa watumishi walio wengi.

"Tumeleweshwa manufaa ya mfuko kwa watumishi pindi watakapostaa, na kuondoa dhana potofu iliyojengeka kwa watumishi wengi na kuuona mfuko kama ni unyonyaji jambo ambalo si sahihi, elimu hii ni muhimu na inapaswa kutolewa kwa watumishi mara kwa mara". Amesisitiza Msumi

Naye Mwanasheria wa Halmashauri ya Arusha, Mhudini Lesirwa, ameomba marekebisho ya sheria ya fao la uzazi kupatiwa wanaume pindi wenza wao, wanapojifungua kwa kuwa, wapo wanaume ambao ni watumishi lakini wenza wao si watumishi.

"Mfuko unapaswa kufikiria kutoa fao la uzazi kwa wanaume ambao wenza wao si watumishi, ili nao wafaidi mfuko huo sawa na wanawake, kwa kuzingatia kila mwanachama ana haki sawa bila kuzingatia jinsi yake". Ameweka wazi Lesirwa

Kikao kazi hicho, kimetoa nafasi kwa watumishi kuuliza maswali mengi na kupatiwa majibu, jambo ambalo limejenga uelewa wa pamoja kati ya wwatumishi na Mfuko hususani kwenye suala zima la kikokotoo.





# MILIONI 200 ZAKAMILISHA UJENZI WA NYUMBA 4 ZA WATUMISHI WA AFYA

**Na Elinipa Lupembe**

Katika kutekelazaji wa mikakati ya serikali ya kuboresha miundo mbinu kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya, serikali imefanikiwa kuwekeza kwenye ujenzi wa nyumba za watumishi lengo likiwani kuhakikisha wananchi wanapata huduma za afya katika maeneo yao na kwa muda wote.

Katika mwaka wa fedha 2021/2022, halmashauri ya Arusha ilipokea kiasi cha shilingi milioni 200 fedha kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 4 za watumishi kwenye vituo 4 vya Afya vilivyopo maeneo ya pembezoni.

Mkurugenzi Mtendaji halmashauri ya Arusha Seleman Msumi, amebainisha kuwa kiasi hicho cha fedha kimetumika kujenga nyumba 4 za watumishi wa afya kwa gharama ya shilingi milioni 50 kwa kila nyumba.

"Fedha hizo zimejenga nyumba za watumishi kwenye maeneo ambayo watumishi hawakuwa na mahali pa kuishi na kulazimika kuishi mbali na vituo vyao vya kazi, nyumba hizi zimejengwa kwenye zahanati za LoovLukuny na Ilkerini kata ya Kisongo, zahanati ya Ilkirevi kata ya Oltoroto, na kituo cha Afya Nduruma".Amefafanua Mkurugenzi Msumi

Naye Mkuu wa Idara ya Mipango, Anna Urio, amesema kuwa fedha hizo ni utekelezaji wa malengo ya bajeti ya halmashauri ya mwaka wa fedha 2021/2022 ulioishia June 2022 wa kuboresha mazingira ya watumishi ili kuongeza tija na ufanisi katika kazi.

Naye Mganga Mfawidhi zahanati ya Ilkirevi kata ya Olturoto, Atu Sanga, amsema kuwa uwepo wa nyumba ya mtumishi wa afya, utaongeza tija na ufanisi wa kazi, ikiwa nipamoja na kutoa huduma za afya kwa masaa 24.

"Mtumishi akiishi eneo la kazi inampunguzia gharama za kulipa kodi ya nyumba lakini inatuwezesha kutoa hudma za emergence hasa nyakati za usiku, wagonjwa wanakuwa na uhakika wa kupata matibabu". Amefafanua Mganga huyo Mfawaidhi.



Hata hivyo Diwani wa kata ya Olturoto, ameishukuru seikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Mheshimwa Samia Suluhu Hassan, kwa utekelezaji wa Ilani ya CCM, katika sekta zote hususani sekta ya afya, sekta ambayo ni muhimu kwa afya za wananchi.

"Ninampongeza na kumshukuru mheshimiwa Rais, kwa niaba ya wananchi wa Olturoto, ujenzi wa nyumba ya mtumishi ni wazi utaongeza tija katika utendaji wa kazi lakini uwanda mpana wa upatikanaji na utoaji wa huduma za afya kwa wananchi sambamba na kupunguza vifo vya wanawake na watoto" Amesisitiza Mhe. Simon

Ujenzi wa miundombinu ya afya ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 -2025 wa kuongezeka vituo kutolea huduma za afya nchini ikiwemo zahanati, vituo vya afya na hospitali pamoja na nyumba za wahudumu wa afya.






# 'FATHER ON DUTY' KUPINGA ULAWITI KWA WATOTO WA KIUME SHULE ZA MSINGI

**Na Elinipa Lupembe**

Kinababa sita wa Kamati ya Kutetea na Kupinga ukatili wa kingono na ulawiti kwa watoto wa kiume, halmashauri ya Arusha 'Father on Duty' wakiwa kwenye mdahalo na wanafunzi wavulana wa maabara ya kupinga ukatili wa kingono dhidi yao (Boy's Vac Lab), shule ya Msingi Naurei.

Kina baba hao, wamekutana na klabu ya watoto wavulana na kufanya mdahalo uliambatana na utoaji wa elimu kwa watoto hao juu ukatili wa kingono husani ulawiti kwa watoto wa kiume.

Mwenyekiti wa Kamati ya 'Father on Duty' Fanuel Sirikwa, ameelezea namna ya matukio ulawiti kwa wavulana yalivyoongezeka kwa kasi na kuwataka watoto kujitambua na kuchukua hatua ya kupinga vitendo hivyo kwa nguvu kubwa.

Aidha amewataka watoto hao, kupinga vitendo hivyo na kutoa taatifa kwa siri endapo watakutana na mtu atakayewashawishi kufanya hivyo ama endapo kuna mtoto au watoto wanafanya vitendo hivyo ili waweze kusaidiwa na kuachana na tabia hizo mbaya.

Hata hivyo wavulana hao wamekiri kufahamu tabia hizo na kuwa zinaendelea kwenye jamii yao, na kuwaomba wazazi na jamii, kuwasimamia watoto wao ili kuwaepusha na madhila hayo mabaya kwa watoto na taifa kwa ujumla.

Nasiri Shaban mwanafunzi wa darasa la VI shule ya Msingi Naurei, amewataka watoto kupinga vitendo hivyo haramu, kwa kuepuka vishawishi vya kuoewa zawadi ndogondogo, na kuimba jamii kuendelea kutoa elimu kwa watoto juu ya madhara ya ulawiti kiafya, kiakili na kijamii.

Halmashauri ya Arusha kwa kushirikiana na shirika la CWCD, linatekeleza mradi wa kupinga ukatili wa kingono na ulawiti kwa watoto wa kiume, kwa kuanzisha maabara za wavulana 'Boy's Vac Lab' katika shule sita za msingi za Naurei, Moivo, Ilboru, Olturoto, Kiranyi na Ngaramtono kwa ufathili wa Foundation for Civil Society.






# DSW NA KITUO SALAMA CHA WASICHANA KIJIJI CHA IMBIBYA

**Na Elinipa Lupembe**

Katika kuimarisha harakati za kupinga ukatili kwa wasichana, Shirika la DSW limejenga Kituo Salama cha Wasichana kijiji cha Imbibya kata ya Mwandet, halmashauri ya Arusha lengo likiwa ni kuwapa eneo wasichana la kuweza kukaa na kubadilishana uzoefu, kujifunza stadi za maisha katika kasuala mbalimbali ya vijana.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kituo hicho, mkurugenzi wa shirika la DSW, Peter Owaga, amesema kuwa, kupitia mradi wa Binti na Maendeleo (BIMA), shirika limekuwa likifanya shughuli mbalimbali na wasichana, na hatimaye kuamua kuwajengea eneo la kudumu la kukutania na kupata mafunzo kwa uhuru, utulivu na kwa mapana zaidi.

Jengo hili litatumika kama darasa na maktaba ya kutoa mafunzo kwa wasichana na vijana, ambapo wasichana wa rika balehe watakutanishwa na watalamu wa kada tofauti na kuwapa elimu ya stadi za maisha, kujitambua na kukabiliana na ukatili wa kijinsia, Afya ya uzazi kwa vijana, uongozi, ujasiriamali na namna ya kujikwamua kiuchumi.

"Kituo kitawapa fursa vijana ya kukaa pamoja na kubadilishana uzoefu masuala ya ujana na ukatili, lakini zaidi kuwakutanisha na watalamu watakaowaelimisha namna ya kukabiliana na changamoto za ujana ikiwemo ukatili na elimu ya ujasiriamali" . Amefafanua Mkurugenzi Mbego.

Naye mgeni rasmi na Afisa Maendeleo Mkoa wa Arusha, Erena Materu, licha ya kulishukuru shirika hilo kwa kushiriki kutekeleza malengo ya Serikali kwa kuwekeza nguvu zaidi kwenye vipaumbele vyake, na kuwataka wananchi wa Imbibya hususani vijana kutumia kituo hicho ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

"Vijana wa Imbibya mna bahati san, halmashauri ina vijiji vingi lakini kituo kimejengwa kwenu, kazi kwenu kutumia kituo hicho na watalamu watakao kuwepo, mkikitumia vizuri na kuleta matokeo mazuri, na vijiji vingine vitajengewa vituo hivi, tunawategemea mkawe mfano wa vijana wa 'Arusha DC' na mkoa mzima wa Arusha." Amebainisha Erena

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Arusha, Afisa Maendeleo ya Jamii - Dawati la Jinsia, Rovil Nguyaine, ameahidi kukisimamia kituo hicho kiweze kuwa endelevu hata pale mradi wa shirika utakapofika mwisho kwa kuhakikisha watalamu wanafika kituoni hapo kutoa huduma huku akiwasisitiza vijana kuhakikisha wanatumia kituo hicho ipasavyo.

Hata hivyo wananchi wa kijiji hicho, wamelishukuru shirika na halmashauri kwa kuhakikisha wanajenga kituo hicho, huku wakithibitisha, kupitia mradi wa Binti na Maendeleo, jamii imeanza kupata uelewa wa madhara ya ukatili wa kijinsia na kuanza kuachana na mila na desturi potofu.

"Kupitia mradi wa Binti na Maendeleo, jamii ya Imbibya imeanza kubadilika, kwa sasa ndoa za utotoni zimepungua, wasichana tunaendelea na masomo, hali ya ukeketaji imeanza kupungua licha ya kuwa bado kuna baadhi ya watu wanafanya kwa siri ila taratibu itafika mwisho" Amefafanua Glory Eliaman, mnufaika wa mradi wa BIMA

Awali DSW imetekeleza mradi wa Binti na Maendeleo kuanzia mwaka 2019 na utakamilika mwishoni mwa mwaka huu 2022, na kufanikiwa kujenga vituo salama kwa wasichana 2 na kuwafikia vijana 4,560, huku wadau 197 wakinufaika kupata elimu kwa ajili ya kwenda kuelimisha na kuhamasisha jamii kupinga ukatili wa kijinsia katika maeneo yao.



# WATAALAMU WA AFYA WATAKIWA KUJIANDAA KUKABILIANA NA UGONJWA WA EBOLA

**Na Elinipa Lupembe**

Mkuu wa wilaya ya Arumeru Mhandisi Richard Ruyango amewaagiza wataalamu wa afya wa halmashauri ya Arusha kufanya maandalizi mapema ili kuweza kukabiliana na ugonjwa wa Ebola ambao hivi karibuni mlipuko wake umetokea katika nchi jirani ya Uganda.

Mhandisi Ruyango ametoa maagizo hayo wakati wa kikao cha kamati ya afya ya msingi halmashauri ya Arusha kilichofanyika katika ukumbi wa Halmashauri hiyo ambapo kimejumuisha viongozi wa dini na mila pamoja na wadau mbalimbali ili waweze kuwa mabalozi wa kutoa elimu hiyo waliyoipata katika maeneo wanapofanyia shughuli zao.

Aidha amesema kuwa pamoja na kuwepo kwa changamoto kama vile upungufu wa rasilimali, dawa, vifaa tiba na kinga, ni muhimu kufanya maandalizi mapema na kuiandaa timu maalum ya ufuatiliaji pamoja kuelimisha Umma juu ya hatari ya ugonjwa huu na namna ya kujikinga.

."Tukumbuke ugonjwa huu hauna tiba bali kinga na unaenea kwa haraka hivyo sisi kama Halmashauri ni vyema kuchukua tahadhari mapema ikiwemo kufanya ukaguzi wa afya kwa wageni wanaoingia nchini hasa katika mipaka isiyo rasmi na kuandaa vituo maalumu kwaajili ya kufanya vipimo vya ugonjwa huo". Alisisitiza Mhandisi Ruyango.

Naye Mjumbe wa kamati ya Afya halmashauri ya Arusha Dkt. Japhet Champanda wakati akiwasilisha taarifa ya utayari wa kukabiliana na ugonjwa huo amesema kuwa, Kila mwananchi anawajibika kuchukua tahadhari za kujikinga na kuwakinga wengine juu ya ugonjwa huu ikiwa ni pamoja na kuepuka kugusa wanyama kama vile popo, nyani, sokwe, tumbili na swala au mizoga ya Wanyama pamoja na kuzingatia usafi wa mazingira na usafi binafsi.

Hata hivyo wajumbe waliohudhuria kikao hicho wameipongeza halmashauri ya Arusha kwa niaba ya Serikali kwa hatua walizokwisha kuzichukua za kukabiliana na ugonjwa huo huku wakishauri elimu iendelee kutolewa katika mikusanyiko ya watu kama vile mikusanyiko ya kimila, makanisani, misikitini, mashuleni na minadani ili wananchi wapate elimu hiyo na wajue namna ya kujikinga.

"Ni vyema kila mtu kwa Imani yake amlilie Mungu ili aweze kutuepusha na janga hili huku elimu ikiendelea kutolewa bila kuleta taharuki kwa jamii ili kila mtu apate uelewa juu ya ugonjwa huu wa Ebola". Alisistiza Mchungaji Pivs Edward Stevan, wa Kanisa la Naioth Gosple Assembly.

Mganga Mkuu Halmashauri ya Arusha Dkt. Petro Mboya ameweka wazi kuwa Halmashauri hiyo kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Arusha wametenga kituo cha afya Moshono kwa ajili ya kufanya matibabu ya wagonjwa waliogundulika na ugonjwa huo pamoja na eneo la TPRI kwaajili ya kuwatenga wahisiwa na waliokuwa karibu na wagonjwa wa Ebola.

Ifahamike kuwa ugonjwa wa Ebola unaosababishwa na Kirusi aina ya Ebola chenye anuwai sita uligundulika kwa mara ya kwanza mwaka 1976 katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Sudan na dalili za ugonjwa huo ni kama vile kupata homa kali ya ghafla, maumivu ya kichwa, Maumivu ya mwili, misuli na viungo, Kuharisha kunakoweza kuambatana na damu, Kutapika damu, Vipele mwilini, Kuvia damu chini ya ngozi au kutokwa na damu puani , mdomoni , machoni na masikioni.




# ASAS YA ZOE AFRICA (TZ) YAWAKWAMUA KIUCHUMI VIJANA YATIMA NA WAISHIO KWENYE MAZINGIRA MAGUMU

**Na Elinipa Lupembe**

ASAS ya kiraia ya ZOE AFRICA (TZ) imefanikiwa kuwaainua kiuchumi na kijamii vijana yatima na wale wanaoishi kwenye mazingira hatarishi, kwa kuwajengea uwezo kulingana na matakwa na matamanio yao pamoja na kuwapa mitaji na vifaa vya ofisi.

ASAS hiyo imefikia hatua hiyo kutokana na changamoto zinazolikabili kundi hilo la vijana wa wenye umri wa miaka 15 - 20, za kukatisha ndoto zao kutokana na kuondokewa na wazazi/mzazi na wenginee kutokana na hali duni za maisha ya familia zao.

Akizungumza wakati wa mahafali ya kuhitimu vijana 156, Mkuu wa wilaya ya Arusha, Mhe. Saidi Mtanda amempongeza mkurugenzi wa ZOE kwa kazi kubwa inayofanywa na shirika hilo, ya kurejesha matumaini ya vijana ambayo yalipotea na pengine kutoweka kabisa.

Mkuu huyo wa Wilaya ameweka wazi kuwa, Serikali inatambua na kuthamini kazi inayofanywa na mashirika yasiyo ya kiserikali, shirika linafanya kazi ambayo ingepaswa kufanywa na serikali, amewapongeza kwa kuunga mkono juhudi za serikali na kuahidi kushirikiana nao.

Ameongeza kuwa, kazi hii si kwa mujibu wa serikali pekee bali ni kazi ya Mungu, mnafanya kazi ya kuwaokoa vijana waliokata tamaa kutoka kwenye wimbi la kihalifu, uzururaji na uvutaji bangi na kuwa vijana wenye heshima kwa jamii na Taifa, malipo yake mtayapata kwa Mungu na si hapa duniani.

"Kundi hili la vijana 156, bila ZOE lingekuwa kwenye hali gani kimaisha, mmetuondolea vijana wasiokuwa na mwelekeo na kuwaleta kwenye kundi la vijana, watakaokwenda kulijenga Taifa la Tanzania, ". Amesisitiza Mhe. Mtanda

Akiwasilisha taarifa ya shirika hilo, Mkurugenzi wa ZOE AFRICA (TZ), Mchungaji Trice Shumbusho, amesema kuwa, katika maafali hayo, jumala ya vijana 150,wamehitimu baada ya kupata mafunzo kwa muda wa miaka mitatu na kufanikiwa kuwapa ujuzi na maarifa, ambao tayari wameshaweza kujitegemea kwa kuanzisha biashara.

"Wahitimu wa leo, wamejengewa uwezo na tayari wameweza kuanzisha biashara kwa kufungua ofisi zao, huku ZOE ikiwapatia vifaa vya ofisi pamoja na pesa ya kodi ya miezi mitatu ya awali, lakini shirika litaendelea kuwasimamia kwa muda mpaka hapo tutakapoona biashara zao zimesimama vizuri".Amefafanua Mkurugenzi huyo

Hata hivyo wahitimu hao, licha ya kulishukuru shirika hilo kwa kuwaleta pamoja, kuwatunza, kuwapa ujuzi na maarifa pamoja na kuwapatia vifaa vya ofisi, jambo ambalo wamekiri ni neema ya Mungu kwa ZOE kuwafanyia huduma hiyo yenye thamani katika maisha yao na familia zao.

Edna Lesikari mkazi wa Mlangarini, amekiri kuwa awali alikuwa na ujuzi mdogo sana wa kushona, lakini ZOE wamempa mafunzo ya ushonaji pamoja na mashine ya cherehani ambapo tayari anamiliki ofisi yake na sasa anauwezo wa kushoma hadi nguo za kiume.

"Nilikuwa na fani ya ususi, lakini sikuwa na mtaji wala vifaa, ZOE wameniwezesha kujifunza fani hiyo kwa ngazi ya juu na kunipa vifaa vilivyoniwezesha kufungua saloni yangu, wakanipa mtaji, ambapo sasa ninauwezo wa kujitegemea, kujikumu kimaisha na kuwahudumia ndugu zangu" . Amesema mwanafunzi Rehema Lucas

Naye Veronica Samson amebainisha kuwa hapo awali hakuwa na uhakika na maisha yake, aliishi kwa kufanya vibarua kwa mama lishe, ZOE imemuwezesha kujifunza kutengeneza 'Peanut butter' na kumpa mtaji, unaomuwezesha kuendesha biashara yake, biashara ambayo inamfanya kujiamini,kujithamini na kujiona anao uwezo wa kuishi kwa malengo.

Shirika la ZOE AFRICA (TZ) linafanya kazi mkoani Arusha kwenye halmashauri za Arusha na Jiji la Arusha, lilianza rasmi mwaka 2019 likiwa na vikundi 10 na vijana 256 wakiwa na wategemezi takribani 737 mpaka sasa kuna vikundi 40 vyenye vijana 968.



# KAMATI YA FEDHA YAKAGUA UJENZI WA KITUO KITUO CHA AFYA MATEVES

**Na Elinipa Lupembe**

Wajumbe wa Kamati ya fedha Utawala na Mipango, halmashauri ya Arusha, wakikagua mradi wa ujenzi wa jengo la Wagonjwa wa Nje (OPD) Kituo cha Afya Mateves kata ya Mateves, mradi utakaogharimu kiasi cha shilingi milioni 197.6, mpaka kukamilika kwake.

Mradi huo unategemea kutekelezwa kwa awamu kupitia fedha za Mapato ya Ndani ya halmasahuri, ambapo kwa awamu ya kwanza ulipatiwa shilingi milioni 79.1 zilizotumika kuanza jengo mpaka hatua ya gebo kwa shilingi milioni 74.9.

Akiwasilisha taarifa ya ujenzi wa Jengo hilo, Afisa Mtendaji wa Kata ya Mateves Muyai Kivuyo ameweka wazi kuwa wamepokea kiasi cha shilingi milioni 30 ikiwa ni awamu ya pili ya utekelezaji, utakaohususha shughuli za upauaji wa jengo hilo.

"Katika utekelezaji wa mradi huu wananchi wamekuwa wakichangia maji wakati wote wa ujenzi na baadaye wameahidi kitachangia gharama za kuunganisha maji kwenye jengo kutoka Mamalaka ya maji"Amefafanua Mtendaji huyo.

Aidha wajumbe hao wa Kamati wameridhishwa na utekelezaji wa mradi huo,na kuwataka viongozi wa kata hiyo, kutafuta wadau watakaowezesha kuongeza nguvu katika ujenzi huo, pamoja na kupanda miti katika kituo hicho ili kutunza mazingira.

Diwani wa Viti Maalum Mhe. Grace Seneu ameupongeza uongozi wa kata na wananchi wa kata hiyo kupitia kamati za ujenzi, kwa kusimamia vizuri mradi huo unaonesha thamani ya pesa 'value for money', kwa kuangalia hata kwa macho.

Naye Diwani mwenyeji wa kata ya Mateves Mhe. Fredy Lukumay licha ya kuwashukuru wajumbe kwa kutembelea mradi huo, amebainisha kuwa ujenzi wa Kituo hicho cha afya unategemea kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wa kata ya Mateves na majirani zake.

"Ujenzi huu unakwenda vizuri, kwa kuwatumia wanakamati ambao ni wastaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kusimamia ujenzi na wanafanya kwa uadilifu mkubwa kulingana na kiapo walichoapa kulitumikia taifa lao".Amesisitiza Mheshimiwa Diwani.

Ujenzi wa huo wa Kituo kipya cha Afya, ni utekelezaji wa malengo ya Serikali ya Awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan wa kusogeza huduma za afya karibu na wanachi kwa kuhakikisha kila kata inakuwa na kituo cha Afya chenye hadhi.





# SERIKALI YAKABIDHI VITI MWENDO KWA WANAFUNZI WENYE ULEMAVU

**Na Elinipa Lupembe**

Serikali ya awamu ya sita, kupitia halmashauri ya Arusha imekabidhi viti mwendo vinne kwa wanafunzi wenye ulemavu kutoka shule nne zenye vitengo vya elimu maalum, viti ambavyo viwarahisishia wanafunzi hao shuguli zao binafsi na zili za kimasomo kwa uhuru na amani.

Akizungumza wakati akikabidhi viti mwendo hivyo, kwa walimu wakuu na wazazi wa watoto hao, Mkurugenzi Mtendaji halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi amesema kuwa, msaada huo umepunguza changamoto ya watoto hao kutembea hasa wakiwa katika mazingira ya shule kutokana uwezo wao mdogo wa kutembea, jambo ambalo lilisababisha udhaifu katika kujifunza na kufundishika wawapo shuleni.

Aidha Mkurugenzi Msumi ametumia fursa hiyo kuwakaribisha wadau mbalimbali kujitokeza kusaidia wanafunzi wengine wenye uhitaji wa namna hiyo ili watoto hao waweze kutimiza ndoto zao.

"Tuna uhitaji mkubwa wa vifaa kwa ajili ya kuwahudumia hawa watoto wawapo shuleni, hivyo nitoe wito kwa yeyote atakayeguswa kutoa msaada akaribie katika ofisi zetu za halmashauri au katika mojawapo ya shule zenye watoto wenye uhitaji wa namna hiyo ili waweze kutoa msaada huo". Alisisitiza Mkurugenzi Msumi.

Hata hivyo wazazi wa watoto hao waliopatiwa msaada, wameishukuru serikali kwa kuendelea kuwakumbuka wahitaji kwa kuwa sasa watoto hao wataendelea kupata elimu bila changamoto iliyokuwa inawakabili hapo awali ya kukaa pamoja na kusogea kutoka sehemu moja hadi nyingine.

"Ninamshuru Rais Samia Suluhu kwa kunipatia hiki kiti ambacho kitanisaidia kusoma bila changamoto, mama alinibeba kunipeleka shuleni, alikuwa anachoka sana, na wakati mwingine hakunipeleka, naamini nitatimiza ndoto yangu ya kuwa Mhasibu". Amesema Catherine Paul, mtoto mwenye ulemavu wa darasa la 3 shule ya msingi Naurei

Kwa upande wao walimu wakuu wa shule hizo wameishukuru na kuipongeza serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwakumbuka na kuwajali watoto hususani wenye mahitaji maalum na kuahidi kushirikiana na wazazi wa watoto hao kuvitunza hivyo viti mwendo ili viweze kudumu na kuwasaidia wanafunzi hao kwa muda mrefu.

"Tunatambua na kuthamini kazi kubwa inayofanywa na serikali hasa kwa kutoa fedha ya chakula kila mwezi kwa watoto wenye ulemavu na sasa imeona umuhimu wa kuwaletea viti mwendo, licha ya kuwa uhitaji bado ni mkubwa lakini tumepata sehemu ya kuanzia". Alisema Mwl. Getruda Tarimo, Mwalimu Mkuu shule ya Msingi Naurei.

Awali, halmashauri ya Arusha inakabiliwa na uhaba wa viti mwendo zaidi ya ishirini (20) katika shule nane zenye vitengo vya Elimu Maalum, pamoja na vifaa vingine kwa ajili ya kuwahudumia hao watoto.





# WATENDAJI WA KATA WASAINI MKATABA WA AFUA ZA LISHE

**Na Elinipa Lupembe**

Maafisa Watendaji wa kata 27 za halmashauri ya Arusha, wamesaini mkataba wa upangaji, ufuatiliaji na utekelezaji wa shughuli za Lishe kwenye maeneo ya kata zao, huku wakitakiwa kufanya kazi hiyo kwa kuzingatia malengo makuu mawili, viashiria na vigezo tisa vilivyoainishwa kwenye makataba huo.

Maafisa hao wamesaini mkataba huo baina yao na Mkurugezni Mtendaji halmashauri ya Arusha, Mkuu wa Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, Mganga mkuu pamoja na Mratibu wa Lishe, ikiwa ni hatua ya muendelezo wa uingiaji wa mikataba ya usimamizi wa shughuli za afua za lishe kuanzia ngazi ya Taifa, Mkoa, wilaya na na hatimaye ngazi ya kata na vijiji.

Akizungumza wakati wa zoezi la utiaji saini mikataba hiyo, Kaimu Mkurugenzi Halmashauti ya Arusha, Elizabeth Ngobei ameweka wazi kuwa, mkataba huo una malengo makuu mawili ikiwa ni kufanikisha suala la kuboresha hali ya lishe na kupunguza athari za utapiamlo na kuhakikisha jamii inashiriki ipasavyo kupanga, kutekeleza na kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa mpango wa halmashauri wa afua za lishe.

Amesema kuwa kwa kuzingatia malengo hayo Maafisa Watendaji ambao ni wasimamizi wapaswa kufanya kazi hiyo kwa weledi kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa, kulingana na vigezo na viashiria 9 vilivyoanishwa kwenye mikataba .

"Kila mtu anafahamu umuhimu wa afya bora katika maisha ya binadamu na ujenzi wa Taifa, Serikali imewapa jukumu hili muhimu, nendeni mkalitekeleze kwa umakini mkubwa kulingana na makubaliano, kama kuna changamoto tushirikishane kwa wakati ili kwa pamoja tufikie malengo yaliyokusudiwa na serikali". Amesisitiza Kaimu Mkurugenzi huyo.

Naye Mratibu wa Lishe, halmashauri ya Arusha, Doto Milembe, amefafanua kuwa, Mkataba wa lishe unawataka Maafisa Watendaji wa Kata kuhakikisha wanashirikiana na Maafisa Watendaji vijiji, kufanya kazi hiyo pamoja na kufanya tathmini na kutoa ripoti ya utekelezaji kwa kila mwezi.

"Lishe duni inanikusababisha umasikini katika Taifa kwani hakutakuwa na Jamii inayoweza kujituma kwa kufanya kazi kutoakana na watu wengi kuathiriwa na utapiamlo, viongozi wenzangu tupambane kutokomeza utapiamlo katika maeneo yetu,,ili kuwa na watu wenye afya bora"Amesisitiza Mratibu huyo wa Lishe.

Nao Maafisa Watendaji wa kata, wameahidi kwenda kufanyia kazi maelekezo yote kama yalivyo malengo yake kwa kuzingatia vigezo na viashiria vilivyoainishwa kwenye mkata, ikiwa ni pamoja na kuifanya agenda ya kudumu kwenye vikao vyote vya kisheria.

Afisa Mtendaji wa Kata ya Bwawani Simon Kaaya amebainisha kuwa, wao kama watendaji wanalo jukumu kubwa la kuutekeleza mpango huo kwa vitendo kwa kuwa unawahusu wananchi moja kwa moja ambao wako chini ya mamlaka zao za vijiji na vitongoji.

"Mpango wa lishe ni muhimu kwa kuwa tunakwenda kuandaa wananchi wenye afya bora ambayo ni nguvu kazi ya taifa, tutatumia majukwaa yote kutoa elimu kwa makundi kwa kushirikiana na wahudumu wa afya ngazi ya jimii na kuhakikisha unakuwa na matokeo chanya" Amesisitiza Kaaya.

Ifahamike kuwa mkataba wa Lishe ni mkakati wa Kitaifa ambao ulisainiwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan jijini Dodoma na baaye kusainiwa na wakurugenzi wa hamashauri kupitia ofisi ya Mkuu wa mkoa na hatimaye, kusainiwa na halmashauri ya Arusha.



# SALAM ZA OFISI YA MKUU WA MKOA KWENYE MKUTANO BARAZA LA MADIWANI

**Na Elinipa Lupembe**

Ofisi ya Mkuu wa mkoa wa Arusha imetoa salamu kwa Wajumbe wa Baraza la Madiwani, halmashauri ya Arusha, wakati wa mkutano wa kujadili taarifa za robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Akitoa salam hizo kwa niaba ya RAS mkoa wa Arusha, CPA. Ramadhani Madegeka ameeleza kuwa, kama ilivyo malengo ya mkoa ni ukusanyi wa mapato, madiwani na wataalamu mnatakiwa kushirikiana katika suala zima la ukusanyaji wa mapato, halamshauri na mkoa uweze kufikia malengo tuliyojipangia kwa mwaka.

"Bila kukusnaya Mapato hatutaweza kufikia malengo tuliyojipangia, niwatake waheshimiwa kuonheza nguvu kayika ukuapsanyaji wa mapato, hadi kufikia mwezi Oktoba, halmashauri imekusanya shilingi bilioni 1.2 sawa na asilimia 26 kutoka kwenye makisio ya shilingi bilioni 4.8 kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ili kufikia 100 % lazima nguvu iongezeke".

Aidha amewataka waheshimiwa Madiwani kushiriki katiaka usimamizi wa miradi ya maendeleo, kwa kuwa kwa robo ya kwanza serikali kuu imetoa fedha nyingi za kutekelza miradi pamoja na asilimia 40 ya mapato ya ndani, hivyo madiwani mnawajibu wa kuzisimamia fedha hizo na miradi iweze kukamilika kwa wakati kwa kuzingatia ubora unaoendana na thamani ya fedha.

Mkoa unasisitiza kushitikiana kwa pamoja watalamu, madiwani na wananchi kwenye usimamizi wa miradi, kwa taratibu za matumizi ya force akaunti.

Serikali imetoa fedha za nje ya bajeti, milioni 760 za ujenzi wa madara 38 ya kidato cha kwanza mwaka 2023, madarasa yanatarajia kukamilia mwanzoni mwa mwezi Disemba, ushiriki wa madiwani ni wa muhimu sana"Amesisitiza Madegeka.

Aidha amewataka madiwani kuzingatia suala la utawala bora kwamba kila Diwani anatakiwa kufuatilia mipango yote na utekelezaji wake na kuhakikisha kila kilichopangwa kufanyika kifanyike kulingana na bajeti iliyopangwa

Madiwani mnatakiwa kuzingatia mgawanyo wa matumizi kulingana na kanuni za matumizi ya mapato ya ndnai ya asilimia 40 utekelzaji wa miradi, asilimia 10 za mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu,na asilimia 50 ya matumizi ya kawaida, ili kuepeuka migogoro isiyokuwa ya lazima na matumizi yasiyozingatia sheria.





# NGO's ZATAKIWA KUIBUA MIRADI KWA KUZINGATIA MAHITAJI YA JAMII HUSIKA

**Na Elinipa Lupembe**

Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO's), halmashauri ya Arusha, yametakiwa kuibua na kutekeleza miradi inayozingatia mahitaji ya jamii husika kwa kujikita katika kutekeleza vipaumbele vya serikali huku yakizingatia sheria na taratibu za uendeshaji wa mashirika nchini.

Rai hiyo imetolewa na Mkuu wa wilaya ya Arumeru, Mhandisi Richard Ruyango, wakati wa kikao cha kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli zilizofanywa na Mashirika hayo kwa kipindi cha robo ya kwanza, kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano halmashauri ya Arusha.

Mkuu huyo wa wilaya licha ya kuridhishwa na taarifa za utekelezaji zilizowasilishwa na mashirika hayo, ameyasisitiza mashirika hayo, kufanya kazi kwa weledi kwa kuzingatia mahitaji ya wananchi na vipaumbele vya serikali kisekta.

"Nimeridhishwa na kazi zinazofanyika, kwa kuwa zimejikita kutatua changamoto za jamii kwenye sekta ya elimu, afya, kilimo, lishe, biashara na ujasiriamali, uhifadhi na utunzaji wa mazingira, kupambana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto, lakini zaidi napongeza suala la kupambana na mmea hatari wa gugu karoti". Amebainisha Mhandisi Ruyango.

Aidha ameyaagiza mashirika hayo kuandaa mikakati ya kuanza kutoa elimu kwa makundi ya viongozi ili kuwajengea uwezo wa kuwa na maadili ya uongozi ili kuwa na viongozi wanaozingatia mustakabali mzima wa utawala bora kwa jamii.

Hata hivyo Mkuu huyo wa wilaya ameweka wazi kuwa, serikali inatambua na kuthamini kazi zinazofanywa na mashirika hayo, ikiwa ni utekelezaji wa malengo ya serikali ya kuwahudumia wananchi, kazi ambazo zilipaswa kufanywa na serikali.

Nao wawakilishi wa mashirika hayo wameishukuru serikali kwa kuyaamini mashirika na kushirikiana nayo katika kutoa huduma za jamii kwa niaba ya serikali zaidi wakimpongeza mheshimwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutambua na kuthamini kazi zinazofanywa na ASAS za kiraia huku akiisisitiza serikali kuweka mazingira wezeshi kwa mashirika.

Herieth Raju mwakikishi wa shirika la GLAMI ameishukuru halmashauri kwa ushirikiano na amewataka wadau wanaofanya kazi zinazofanana, kushirikiana na kufanyakazi kama timu pamoja na kubadilishana uzoefu kwa kuweka mikakati ya kuhudumia jamii kwa pamoja ikiwa ni kuhamasisha na kuwajengea wananchi uwezo wa kujitegemea.

"Kwa mfano Mashirika yanayosupport wanafunzi kupata chakula shuleni, wawajengee uwezo wazazi wa kutambua kuchangia chakula cha watoto wao shuleni ni jukumu lao, badala ya kuwapa chakula cha bure kwa miaka yote, jambo linalowafanya baadhi ya wazazi kubweteka na kuona kama hilo si jukumu lao". Amesema Herieth

Naye Msajili wa Mashirika halmashauri ya Arusha Ahadi Mlay, ameyapongeza mashirika hayo kwa ushirikiano sambamba na uwasilishaji wa taarifa za robo kwa wakati na kuwasisitiza, kuhakikisha wanatekeleza shughuli zao kama maandiko ya miradi yao yanavyoelekeza na si vinginevyo.

Awali kikao hicho ni kikao cha robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kipindi cha Julai - Septemba 2022 ni cha kawaida kwa mujibu wa kanuni na miongozo ya serikali za mitaa, inayoyataka mashirika yasiyo ya kiserikali, kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa shughuli zinazofanyika kwa kila robo ya mwaka huku jumla ya mashirika 30 kati ya 38 yamewasilisha taarifa zake.



# WAJUMBE WA KAMATI YA FEDHA WAPONGEZA UJENZI WA BWENI LA WANAFUNZI SEKONDARI KIMNYAKI

**Na Elinipa Lupembe**

Wajumbe wa Kamati ya Fedha Utawala na Mipango, halmashauri ya Arusha, wamewapongeza wananchi wa Kimnyaki kwa kujitoa kuanza ujenzi wa bweni la wasichana shule ya sekondari Kimnyaki, lenye uwezo wa kulaza wanafunzi 80.

Pongezi hizo zimetolewa wakati wajumbe wa kamati hiyo walipofanya ziara ya kukagua shughuli za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa robo ya kwanza mwaka wa fedha 2022/2023

Akiwasilisha taarifa ya mradi huo, mkuu wa shule ya sekondari Kimnyaki, Mwl Maria Chami, amesema kuwa mradi huo, ulianza kwa nguvu za wananchi kwa kufanya harambee na kupata jumla ya shilingi milioni 19 ambazo zilianza ujenzi wa msingi.

Mwalimu Maria amesema kuwa mradi huo uko katika hatua za awali na kukamilika kwakwe kunategemea kugharimu shilingi milioni 150.8, huku halmashauri imetoka shilingi milioni 10 kupitia mapato yake ya ndani, na kuahidi kuendelea kutoa fedha hizo kwa mujibu wa bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2022, fedha ambazo zitaongeza nguvu za kuendeleza ujenzi wa bweni hilo.

Naye Diwani wa kata ya Kimnyaki Mhe. Eliakimu Marivei, amebainisha kuwa, wananchi wa Kimnyaki waliamua kuunganisha nguvu kujenga bweni la wasichana shuleni hapo, kwa kuzingatia usalama wa mtoto wa kike anayekabiliwa na changamoto za vishawishi vinavyosababisha mimba na ndoa za utotoni.

"Tumeamua kujenga bweni, kumuwezesha mtoto wa kike kusoma na kutimiza ndoto zao bila vikwazo, kiwa ni utekelezaji wa malengo ya Serikali ya kuboresha miundombinu ya elimu nchini". Amefafanua Mhe.

Hata hivyo wajumbe wa kamati ya fedha wamepongeza wananchi wa Kimnyaki pamoja kurudhishwa na maendeleo ya ujenzi, na kumuagiza mkurugenzi wa halmashauri kuendelea kutoa fedha kwa mujibu wa bajeti ili kuunga mkono juhudi za wananchi wa Kimnyaki.

Makamu Mwenyekiti Halmashauri ya Arusha, Mhe. Selina Mollel, amewapongeza wananchi wa kata ya Kimnyaki kupitia Mheshimiwa Diwani wao, na kuwataka wengine kuiga mfano huo na kuwataka madiwani kuunga mkono juhudi hizo kwa manufaa ya wasichana na wananchi wa halmashauri ya Arusha.





# WASIMAMIZI WA MRADI WA UJENZI WA MADARASA 38 WAPEWA SOMO

**Na Elinipa Lupembe**

Wasimamizi wa mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa shule za sekondari, halmashauri ya Arusha, kupitia fedha za serikali shilingi milioni 760, wametakiwa kutekeleza miradi hiyo kwa kuzingatia kanuni, sheria na taratibu za matumizi ya fedha za Umma.

Wasimamizi hao wamepata fursa hiyo, wakati wa kikao kazi maalum, chenye lengo la kukumbushana sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya matumizi ya fedha za Umma, katika utekelezaji wa miradi ya serikali, kikao kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa halmashauri hiyo, mwishoni mwa wiki iliyopita.

Mkurugenzi Mtendaji, halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi amewataka wasimamizi hao, kushirikiana kwa pamoja kama timu katika utekelezaji wa mradi huo wa ujenzi vya vyumba vya madarasa na kuwasisitiza kufuata taratibu zote ikiwa ni pamoja na utunzaji wa taarifa zote muhimu na kukamilika kwa wakati ili kufikia lengonla kuwapokea wanafunzi wa kidato cha kwanza 2023.

"Fedha zimeshaingia kwenye akaunti za shule, tunakwenda kujenga vyumba 38 vya madarasa kwa milioni 20 kwa darasa likiwa na madawati 40, kupitia 'Force Akaunti' na kutumia ramani zilizotumika kwenye program ya EP4R, ndani ya siku 75, ujenzi uwe umekamilika, hakikisheni tunakamilisha kwa wakati". Ameagiza Mkurugenzi Msumi

Amefafanua kuwa Serikali imeweka taratibu za matumizi ya 'Force akaunti' ikiwa ni pamoja na ushiriki wa jamii katika ujenzi, hivyo ni wajibu wa kila mwenye dhamana ya kusimamia mradi kushiriki kutekeleza majukumu yake, lengo likiwa kuongeza uwazi na uwajibikaji wa jamii katika kusukuma gurudumu la maendeleo.

Naye Mkuu wa Idara ya Mipango, halmashauri ya Arusha, Anna Urio, amefafanua kuwa lengo la kikao hicho ni kukumbushana na kuwa na uelewa wa pamoja juu ya taratibu za matumizi ya fedha za Serikali katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa.

"Kila mwenye dhamana anatakiwa kufahamu kiasi cha fedha na idadi ya madarasa, muda wa utekelezaji, kuzingatia ubora wa mradi unaoendana na thamani ya fedha 'value for money', pamoja na ushirikishwaji wa jamii katika utekelezaji wa miradi kabla na wakati wote wa utekelezaji wa mradi". Amefafanua Afisa Mipango Anna.


Naye Mkuu wa Idara ya Ujenzi halmashauri ya Arusha, Mhandisi Nuru Mkwazu, ameahidi kuzingatia hatua za awali ikiwa pamoja na namna ya kupata wakandarasi na wazabuni kupitia ushindani kwa kuzingatia bei halisi ya soko na gharama za mradi pamoja na uteuzi wa kamati za usimamizi wa mradi.

Aidha kaimu Mweka Hazina, halmasahuri ya Arusha, Tido Moiro, amesisitiza kuhakikisha mkandarasi analipa kodi zote za Serikali, pamoja na asilimia 5 ya gharama ya mkataba 'retaintion', fedha ambayo itazuiliwa mpaka kazi itakapokamilika na endapo itatokea tatizo lolote pesa hiyo itatumika.

Hata hivyo walimu hao, wameupongeza uongozi wa halmashauri, kwa kikao kazi hicho ambacho wamekiri kina manufaa kwao, kutokana na ukweli kwamba, utekelezaji wa miradi hiyo unahitaji usimamizi imara wenye tija ili kufikia malengo ya serikali ya kuhakikisha wanafunzi wa kidato cha kwanza wanaingia darasani mapema Januari 2023.

Awali, kikao kazi hicho kimejumisha Maafisa Watendaji wa Kata, Maafisa Elimu kata na Wakuu wa shule zenye miradi, inayotekelezwa na fedha za pochi la mama.

VYUMBA 5 VYA MADARASA NA OFISI 1 SHULE YA SEKONDARI KIRANYI




VYUMBA 4 VYA MADARASA SHULE YA SEKONDARI MRINGA




VYUMBA 4 VYA MADARASA NA OFISI 2 SHULE YA SEKONDARI EINOTH




VYUMBA 3 VYA MADARASA SHULE YA SEKONDARI LIKAMBA




VYUMBA 3 VYA MADARASA SHULE YA SEKONDARI SAMBASHA




VYUMBA 3 VYA MADARASA SHULE YA SEKONDARI OLDADAI




VYUMBA 2 VYA MADARASA NA OFISI 1 SHULE YA SEKONDARI OLTUROTO




VYUMBA 2 VYA MADARASA NA OFISI 1 SHULE YA SEKONDARI LOSINONI




VYUMBA 2 VYA MADARASA NA OFISI 1 SHULE YA SEKONDARI OLJORO



VYUMBA 2 VYA MADARASA NA OFISI 1 SHULE YA SEKONDARI OLOMITU




CHUMBA 1 CHA DARASA SHULE YA SEKONDARI ENDEVES




CHUMBA 1 CHA DARASA SHULE YA SEKONDARI LOSIKITO




CHUMBA 1 CHA DARASA NA OFISI 1 SHULE YA SEKONDARI OLEMEDEYE




CHUMBA 1 CHA DARASA SHULE YA SEKONDARI OLDONYOWAS




CHUMBA 1 CHA DARASA SHULE YA SEKONDARI OSILIGI




CHUMBA 1 CHA DARASA SHULE YA SEKONDARI MUKULAT




CHUMBA 1 CHA DARASA SHULE YA SEKONDARI BANGATA




CHUMBA 1 CHA DARASA SHULE YA SEKONDARI MUSA



# FAHARI YETU

## HALMASHAURI YA ARUSHA

enaboishu

FM RADIO 101.3

Imetolewa na
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Halmashauri ya Arusha


**Mhariri Mkuu:**
Seleman H. Msumi
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Arusha

**Mhariri Msaidizi:**
Elinipa J. Lupembe
Afisa Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Arusha

**Msanifu:**
Daniel Z. Gitaro
danielgitaro@gmail.com



Mawasiliano; S. L. P 2330, Arusha | Barua pepe : ded@arushadc.go.tz


**Fuatilia kurasa zetu za Mitandao ya kijamii kwa habari na matukio mbalimbali zinazoenesha utekelezaji wa shughuli za Maendeleo katika Halmashauri ya Arusha kama zilivyoainishwa hapa chini.**

www.arushadc.go.tz | Arusha District Council | arusha_district_council